SUPA JACKPOT
TZS. 1,096,041,286
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Papa** Francis alazwa hospitalini

UKURASA 19


BUFE
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
HIFADHI KITULO NA UPEKEE WAKE
UCHUMI
**Bosi COSTECH: Miaka miwili kiserikali, tunaneemeka kwa teknolojia uchumi**
• Yabeba tenda kuhudumia nchi kiufundi

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Machi 31, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581266


www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Neema Tanzania

**• Ni** ziara ya Kamala, Dola milioni 560 kumwagwa, biashara kupaa...

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, wakati wakizungumza na waandishi wa habari, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **Picha ndogo:** Makamu wa Rais, Kamala Harris akipunga mkono kwa furaha baada ya kuwasili katika ukumbi wa Kikwete Ikulu. **PICHA: IKULU**



## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### TAKUKURU YABAINI MIRADI YA TRIL. 5.6/- UTEKELEZAJI WAKE DUNI



TAASISI ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU), kwa kipindi cha 2021/2022 katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo 1,548 yenye thamani ya Sh. trilioni 5.64...

### Utapeli mpya unavyowaliza wafanyabiashara wa Kariakoo

UKURASA 3

# Mahakama: Wabunge, madiwani hakuna kupita bila kupingwa

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA: TUNAHITAJI HESHIMA MOROCCO UK.24

**KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, kabla ya mazungumzo yao, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Wabunge, madiwani hakuna kupita bila kupingwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Masijala Kuu Dar es Salaam imebatilisha vifungu vinavyoruhusu wabunge, madiwani na wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Kijiji au kitongoji kupita bila kupingwa katika uchaguzi.

Vifungu hivyo ni kinyume na Katiba, vinakiuka Ibara ya 21(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji John Mgetta, Jaji Dk. Benhaji Masoud na Jaji Edwin Kakolaki baada ya kupitia maombi ya kupinga vifungu hivyo vya Sheria ya Uchaguzi na majibu ya wajibu maombi.

Naibu Katibu Mkuu wa ACT - Wazalendo, Joram Bashange, aliwasilisha maombi dhidi ya Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika maombi yake Bashange aliambatanisha hati ya kiapo aliyoapa na mjibu maombi alijibu akiambatanisha na hati ya kiapo kinzani kilichoapwa na Fausta Mahenga.

Katika maombi yake Bashange anapinga uhalali wa kikatiba wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura. 343 na kifungu cha 45(5) na 13(7) cha Sheria ya Uchaguzi Serikali za Mitaa sura ya 292.

Bashange anadai kwa kuruhusu wagombea wasio na upinzani kama ilivyosemwa hapo awali, vifungu vinavyopingwa vinakiuka haki za raia kupiga kura kuwachagua wawakilishi. Inadaiwa masharti hayo yanakiuka ibara ya 21(1) na (2) na Ibara ya 26(1) ya Katiba.

Kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 21(1) bila kuathiri masharti ya Ibara ya 39, 47 na 67 ya Katiba ya Sheria za nchi kuhusiana na masharti ya kuchagua na kuchaguliwa au kuteuliwa kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, kila raia wa Jamhuri anayo haki ya kushiriki ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sheria.

Ibara ya 21(2) inasema kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi wa mambo yanayomuhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu taifa.

Ibara ya 26(1) inasema kila mtu ana wajibu wa kufuata na kuitii Katiba na Sheria za Jamhuri ya Muungano.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili iliangalia vile vile katika Ibara 76 na 77(1) ya Katiba kuhusu matakwa ya kufanya uchaguzi katika kila jimbo na wananchi kushiriki katika uchaguzi huo kwa kina.

Ibara ya 76 inasema kila baada ya Bunge kuvunjwa kutakuwa na uchaguzi wa wabunge katika majimbo yote ya uchaguzi.

Ibara ya 77(1) ya Katiba inasema wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi watachaguliwa na wananchi kwa kufuata masharti ya Katiba hiyo na vile vile masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba kuhusu wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi.

"Tunakubaliana na mwombaji kwamba sheria iliyotungwa kudhibiti uchaguzi wa wabunge wanaowakilisha maeneo inapaswa kuzingatia maagizo ya Katiba ambayo kwa lazima kutoa haki ya kupiga kura kama njia ya kupata wabunge wa Bunge linalowakilisha majimbo ya uchaguzi," lilisema jopo.

Jopo lilisema katika kupitia Katiba hawakuweza kupata chochote kinachoruhusu utaratibu unaohitaji wagombea ambao hawajapingwa au wasiogombea kuchukuliwa na kutangazwa.

Mahakama inasema kutokana na hoja zilizotangulia mwombaji anayo hoja ya kutosha kuonyesha kuwa masharti yaliyopingwa yanakiuka ya kifungu cha 21 cha Katiba inapoanzisha mambo mapya au hali zinazowabana watu kutumia haki ya kupiga kura kumchagua mgombea aliyependekezwa na chama katika jimbo au kata ambayo kuna mgombea pekee.

Mahakama ilisema katika hoja za wajibu maombi haijaonyesha jinsi masharti yanayopingwa yanavyofaa ndani ya madhumuni yoyote ya utoaji haki, haikuonyeshwa jinsi uokoaji wa gharama za serikali kwa kutojihusisha na uchaguzi na mgombea aliyependekezwa hapigiwi kura kuwa iko ndani ya vipengele vyovyote vya ibara ya 30(2) ya Katiba kama wanavyodai.

Jopo lilisema hata kama imeonyeshwa hivyo, bado Mahakama haijashawishika kwa kuwa mwombaji anachotafuta katika maombi yake ni kuhusu anayelalamikiwa, mfumo huo unaathiri maslahi ya umma.

Pia hawaoni kitu chochote halali ambacho kilikuwa kinakusudiwa kuafikiwa katika sheria hiyo zaidi ya kuanzisha kundi la wabunge na madiwani waliotangazwa kuchaguliwa bila kupingwa. "Kwa kuzingatia upungufu katika hoja za wajibu maombi kuhusu utumikaji wa masharti ya kuokoa gharama, tunakubali kuwa masharti yaliyopingwa hayapo katika ibara ya 30(1) na (2) ya Katiba kama inavyodaiwa na walalamikiwa.

"Tunakubali kuwa vifungu vilivyopingwa vinakiuka Katiba na wajibu maombi hawakuweza kutoa uthibitisho wa kuonyesha kwamba masharti yaliyotajwa ni muhimu na yamo katika kifungu cha 30(2) cha Katiba.

"Katika suala hili, hatuna chaguo lingine isipokuwa kuzingatia ibara ya 64(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kuhusu masharti yaliyopingwa.

"Mahakama inaona hoja zilizowasilishwa zinatosha kuondoa vifungu vinavyopingwa kwa manufaa ya mwombaji.

"Kwa sababu zilizotajwa hapo juu, maombi yanakubaliwa, tunatangaza kwamba masharti ya kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura 343 na vifungu 45(2) na 13(7) vya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, sura ya 292 ni kinyume cha Katiba hivyo basi ni batili kwa kukiuka masharti ya ibara ya 21(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ilivyorekebishwa mara kwa mara," lilisema jopo.

# Marekani yatangaza neema kwa Tanzania

**Na Elizabeth Zaya**

NI neema kwa Tanzania. Ndivyo inavyoonekana kutokana na ziara ya Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, kutokana na ahadi za kutoa misaada ya fedha na kuimarisha biashara kati ya nchi hizo mbili.

Hayo yalibainika jana Ikulu, Dar es Salaam, katika mkutano kati ya kiongozi huyo na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kupitia mkutano huo wa pamoja, Tanzania na Marekani zimetangaza kuanza rasmi majadiliano ya kuimarisha biashara baina yao katika maeneo makuu manne na kwamba Marekani inakusudia kutoa Dola za Kimarekani milioni 560 zikiwa msaada kwa Tanzania katika mwaka wa fedha wa 2023/24.

Majadiliaono hayo ambayo nchi hizo zimefungua ni katika kuimarisha uchumi wa kidijitali, kuyafikia masoko ya Marekani, mabadiliko ya kanuni na mazingira ya biashara na ziara za kibiashara.

Aidha, nchi hizo leo zitatiliana saini makubaliano hayo kupitia wizara zenye dhamana za viwanda na biashara yakilenga pia kushughulikia vikwazo vinavyokwamisha kuongezeka kwa biashara na uwekezaji na kupanua maeneo hayo katika kipindi cha miaka mitatu.

Rais Samia alisema majadiliano hayo yataanzisha vikosi kazi vyenye wawakilishi kutoka Ubalozi wa Marekani nchini na serikali ya Tanzania, vikifuatiwa na mkutano wa mwaka wa wakuu wa taasisi kujadili jinsi ya kukuza na kuimarisha ushirikiano wa kibiashara.

"Hati ya makubaliano itakayotiwa saini kati ya benki ya EXIM ya Marekani na serikali ya Tanzania, itaongeza ushirikiano wa kibiashara kwa kuziwezesha kampuni za Marekani kuleta Tanzania bidhaa na huduma bora za kibunifu na itawezesha upatikanaji wa hadi Dola milioni 500 kugharimia upelekaji wa huduma na bidhaa Tanzania.

"Pia itasaidia upelekaji wa bidhaa na huduma hizo katika sekta mbalimbali hususani miundombinu, usafirishaji, teknolojia ya kidijitali, nishati na miradi ya nishati jadidifu. Pia itasaidia kuimarisha na kuongeza fursa za kiuchumi na kukuza ajira Tanzania na Marekani," alisema.

**MISAADA KIBAO**

Kamala alisema nchi yake inathibitisha azma ya kuhuisha ubia na ushirikiano na Afrika na kujenga dhamana ambayo EXIM imepewa na bunge la Marekani ya kuongeza na kuimarisha uhusiano kati ya wafanyabiashara wa Marekani wanaouza bidhaa na huduma nje ya Marekani na Afrika hasa kusini mwa Jangwa la Sahara.

Miongoni mwa mambo ambayo Marekani imeahidi kupitia kiongozi hiyo kwa Tanzania ni pamoja na kutoa Dola milioni moja kwa ajili ya miradi itakayohimiza kuondolewa kwa vikwazo dhidi ya uhuru wa kujieleza na ule wa vyombo vya habari.

Ahadi nyingine ni kusaidia azma ya Tanzania ya kuimarisha demokrasia kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu mwaka 2025. Kupitia azma hiyo, Marekani imeahidi kutoa Dola 400,000 kusaidia Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), kuwawezesha wadau kujadili zaidi mageuzi ya kidemokrasia na kisheria.

Marekani pia imeahidi kutoa Dola milioni 8.4 kusaidia uzinduzi wa programu ya miaka mitano ya Heshimu Bahari ambayo inalenga kuimarisha uthabiti wa kiikolojia na tija katika mfumo wa ikolojia ya bahari Tanzania. Pia imeahidi kutoa Dola milioni 16 kuwezesha kuzindua mradi wa kilimo tija unaolenga kuwasaidia wakulima, hususani wanawake na vijana.

Pia aliahidi nchi hiyo kutoa Dola milioni 433 katika miaka miwili ijayo kusaidia mapambano dhidi ya Ukimwi, Dola milioni 39 katika mwaka mmoja ujao kupambana na malaria na Dola 600,000 kufanya kazi na kampuni binafsi za mawasiliano ili kupanua huduma ya nishati safi na umeme katika zahanati na vituo 100 vya afya vijijini na miji midogo magharibi, kati na kusini mwa Tanzania.

Ahadi nyingine ni kutoa Dola milioni 26 ili kuimarisha uwezo wa Tanzania kuzuia, kubaini na kukabiliana na milipuko ya magonjwa ya kuambukiza na kushirikiana na Tanzania kupambana na mlipuko wa ugonjwa wa Marburg ambao uliibuka hivi karibuni Kagera.

**PONGEZI KWA SAMIA**

Marekani, kupitia kwa Kamala, ilipongeza jitihada zilizochukuliwa na Rais Samia katika kuimarisha demokrasia na uhuru wa kujieleza na kwamba inaunga mkono kikamilifu ajenda ya Tanzania ya mageuzi ya kidemokrasia.

Alisema Marekani inathibitisha ubia imara kati yake na Tanzania na itaimarisha zaidi ushirikiano katika biashara, jitihada za kutafuta ufumbuzi kuhusu usalama na uhakika wa chakula, ulinzi wa baionuai za majini, uwekezaji kwa wanawake na vijana, afya na demokrasia.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Uwekezaji, Viwanda, Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (wa pili kushoto) na ujumbe wake wakipata maelezo kutoka kwa mtaalamu wa maabara wa Kiwanda cha Tanzania Biotech Products Limited (TBPL) cha Kibaha mkoani Pwani, Jovin Magayane (kushoto), kuhusu namna sampuli mbalimbali zinavyopimwa ndani ya maabara ya kiwanda hicho ili kuzalisha viuadudu vya kuangamiza mazalia ya mbu, walipotembelea jana.
**PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Utapeli mpya unavyoliza wafanyabiashara Kariakoo

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYABIASHARA wa eneo la Kariakoo wamelalamikia kuibuka kwa wimbi la utapeli wa pesa na wizi wa mali unaofanywa na watu wanaodaiwa kuwa ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, hali inayowarudisha nyuma kimaendeleo.

Imedaiwa kwamba watu hao wamekuwa wakiingia katika maduka ya wafanyabiashara hao kwa njia ya kununua mzigo baadaye kuomba kuanzimwa kiasi kidogo cha pesa za Kitanzania na kuacha kiasi kikubwa cha Dola za Kimarekani ambacho baadaye hubainika kuwa ni feki.

Mmoja wa waliokumbwa na utapeli huo juzi, Betty Mmari, anayefanya biashara ya nguo na viatu, alisema walifika wanawake wawili wenye asili ya Congo kwa lengo la kununua nguo. Baada ya kufika walichagua magauni 10 kisha wakamwambia watatumia muda mwingi kuchagua nguo kwa kuwa wamegundua kuwa ana nguo nzuri.

Alisema watu hao walimwomba awaazime Sh. milioni 28 ili wakamalizane na mfanyabiashara mwingine ambaye wameshachagua mzigo na kuuacha kwa makubaliano kuwa watamwachia Dola 20,000 (karibu Sh. milioni 50 za Kitanzania) ili wakirudi waongozane benki kubadilisha na kumlipa fedha zake na za mzigo waliochagua.

"Waliniambia wakishamlipa watarudi ili wachukue pesa zao (Dola 20,000) waende na msaidizi wangu benki wakazichenji kisha wanilipe pamoja na hela ya mzigo waliochagua hapa. Nilikubali kwa kuwa hela wanayoiacha ni kubwa kuliko wanayochukua, halafu sijawahi kusikia utapeli wa aina hii hapa Kariakoo," alisema.

Baada ya kukubaliana walimpa zile Dola 20,000 na akazihesabu na kujiridhisha kuwa zimetimia na ni halali kisha akazirudisha kwenye mfuko kisha akainama kuchukua pesa za Kitanzania ili awape ndipo wakambadilishia ule mfuko na kumpa wenye pesa feki.

"Kumbe walikuwa na mfuko mwingine pembeni wenye hela feki, wakaweka hela halali dola 204 tu (Sh.475,000). Hizo dola 100 waliweka mwanzo halafu dola moja zilikuwa nne wakaziweka katikati na kuzichanganya na makaratasi," alisema.

Mmari alisema baada ya kuwapa hizo pesa, waliacha mzigo waliouchagua na kumwambia watarudi baada ya dakika 15 lakini zikapita saa mbili hawakurudi ndipo akapata wasiwasi na kuziangalia tena zile fedha hatimaye akagundua kuwa ni feki.

Alisema baada ya kugundua aliwashirikisha majirani zake na kwenda kuangalia kwenye kamera na anayehusika na kamera aliwatambua wanawake hao kuhusishwa na utapeli mara kwa mara.

"Hii ni mara ya tano sasa napokea watu wanaokuja kuangalia wahusika waliotapeli kwenye kamera na kila anayekuja tunakamata sura hizi mbili. Hawa watu wameshatapeli watu wengi Kariakoo sema tu watu hawapeani hizi taarifa," alisema John Silayo, mhusika wa kamera.

Mfanyabiashara wa viatu ya kiume katika eneo hilo, Irene Mosha, naye alitoa ushuhuda wa kutapeliwa takribani Dola 20,000 (Sh. milioni 47) na watu hao kwa aina aliyoibiwa Mmari mwaka 2020 hali iliyomwacha na madeni hadi leo.

Alisema ilikuwa ngumu kuwatilia shaka watu hao kwa kuwa Wacongo ni watu wanaoaminika katika soko hilo kutokana na kujijengea uaminifu wa muda mrefu na wafanyabiashara lakini kuna kundi linatumia mwanya huo kutapeli.

"Hawa wanaonekana mtandao wao ni mkubwa pia wanaweza kuwa si Wacongo bali Watanzania wanaojua hiyo lugha. Walikuja wanawake wawili hapa dukani wakaniambia hivyo hivyo niwape pesa wakalipe wakaniachia za kwao nikahesabu. Kitendo cha kwenda kuazima hela kwa jirani ili niongezee wakanibadilishia na kuniachia feki," alisema.

Naye mfanyabiashara Amani Musa alisema mwaka jana alisalimika kutapeliwa dola 15,000 (Sh. milioni 34.9) na watu hao kwa njia hiyo waliofanyiwa wenzake. Alisema kilichomwokoa ni kuwa hakuwa na kiasi walichokuwa wanakitaka badala yake walimwibia nguo 20.

Mfanyabiashara huyo aliliomba Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwatia mbaroni watu hao ili kukomesha vitendo hivyo kwa kuwa vinaelekea kuua uaminifu wa kufanya biashara na wageni.

"Tumefanya biashara na Wacongo, Wamalawi, Wazimbabwe na Wanyarwanda kwa uaminifu mkubwa kwa muda mrefu lakini sasa kuna watu wachache wanataka kuharibu huu uaminifu. Tunaomba Jeshi la Polisi litusaidie katika hili," alisema Musa.

Akizungumzia madai hayo, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Muliro Jumanne, alisema bado hawajapata taarifa yoyote kuhusu suala hilo na kuwataka wale wote waliotapeliwa kutoa taarifa na jeshi litashughulikia.

Alisema polisi wana mifumo imara ya kushughulikia matatizo kama hayo, hivyo taarifa zitakapowafikia watawasaka watu hao na sheria itafuata mkondo wake.

# TAKUKURU yabaini miradi ya tril. 5.6/- utekelezaji wake duni

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU), kwa kipindi cha 2021/2022 katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo 1,548 yenye thamani ya Sh. trilioni 5.64 ikiwamo 237 ya UVIKO-19, ilibaini ina upungufu na utekelezaji wake kuwa duni.

Imetaja upungufu huo kuwa ni kutozingatiwa kwa michoro, ubora wa kazi na vifaa visivyoridhisha kutokana na usimamizi dhaifu huku Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2017 na Kanuni za Mwaka 2013 kutofuatwa.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni, aliyasema hayo juzi, Ikulu, jijini Dar es Salaam, akimkabidhi Rais Samia Suluhu Hassan, ripoti ya taasisi hiyo kwa mwaka 2021/2022.

Alisema kwenye mradi wa UVIKO-19 ilibainika baadhi ya vifaa vilinunuliwa kwa gharama kubwa kuliko zilizopo sokoni, akisema kati ya sababu za miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango ni pamoja na mingi kutekelezwa na 'Force' akaunti, huku maofisa wengi kutojua sheria ya akaunti hiyo.

"Lengo la TAKUKURU ni kufanya ufuatiliaji huu ni kuona fedha, miradi na mtiririko na makadirio ya vifaa vya ujenzi kwenye sekta mbalimbali, ikiwamo miradi ya kimkakati Bwala la Mwalimu Nyerere la uzalishaji umeme pamoja na Reli ya Kisasa (SGR)," alisema Hamduni.

Pia alisema taasisi hiyo iliifikia miradi ya ujenzi wa vituo vya rasilimali kata, 70 ya maji nchini yenye thamani ya Sh. bilioni 60.7 pamoja na inayotekelezwa kwa fedha zilizotolewa kwa kila jimbo, miradi 483 ya Sh. bilioni 248.45, fedha za mpango wa maendeleo na ustawi na UVIKO-19.

Hamduni alisema, katika eneo la utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi hicho ulilenga pia kuzuia rushwa, kutoa elimu, kushirikiana na wadau, tathmini na mwelekeo wa mwaka 2022/2023.

"Uchambuzi wa mifumo 739 ilifanyika kubaini mianya ya rushwa. Tulifanya uchambuzi wa mifumo ya usambazi, udhibiti vifaa vya afya, mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro na Dar es Salaam. Hospitali zilizofikiwa ni Kibon'goto, KCMC, Hospitali ya Kanda ya Mbeya na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), MOI na ORCI. "Pia tulizifikia hospitali za wilaya na vituo na zahanati, MSD...uchambuzi huu ulibaini baadhi ya mifumo ya afya inaathiriwa na kutofuatwa kwa mwongozo wa matumizi ya fedha, kwamba asilimia 50 ya mapato itumike kununulia dawa," alisema Hamduni.

Kadhalika, alisema taasisi ilibaini kuna usimamizi duni pamoja na kutotumiwa mfumo wa kielektroniki katika huduma. "Tulibaini kuna maeneo ya vihatarishi vya rushwa ambayo ni eneo la Forodha, Mapato katika Bandari na ukaguzi bandarini unaofanywa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), TANRODS na Mawasiliano. Tulibaini pia kuna imani potofu kwa watendaji wakiamini bandarini ni mahali pa kuchuma," alisema Hamduni.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
30.03.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatatu tarehe 03.04.2023 kampuni ya **CEVA INTERFREIGHT (T) LTD** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya Dar Es Salaam kuelekea Mzenga gari hizo zenye namba za usajili: **NRB69149/NRB43293, NRB97300/NRB15200, DS00TG GP/NRB23609**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 36.2** |
| **Upana** | - | **mita 7.50** |
| **Kimo** | - | **mita 4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam hadi Mzenga Kupitia Morogoro** Road. Gari zitasafiri muda wa usiku (Kuanzia saa 08:00 usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri) kutoka Bandari ya **Dar Es Salaam mpaka Mlandizi kutoka Mlandizi Kwenda Mzenga** magari yatasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117348702



Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, akiishauri serikali kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wanaojihusisha na vitendo vya ushoga. Wengine ni wajumbe wa taasisi hiyo, Neema Gabriel (kulia) na Precalina Mafole. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wachumi, wanasiasa watoa maoni ripoti ukaguzi CAG, TAKUKURU

**Na Jenifer Gilla**

WATAALAMU wa uchumi na wanasiasa wameishauri serikali kuboresha mifumo iliyoko kwenye taasisi na miradi ya maendeleo nchini ili kudhibiti utendaji kazi wa watumishi na kuepuka hasara za makusudi zinazotokana na kutowajibika ipasavyo.

Sambamba na hilo, wamepongeza mapendekezo ya kutaka kuundwa kwa tume ya kuchunguza fedha za 'plea bargaining' kwamba kwa kufanya hivyo kutaongeza uadilifu kwa watumishi wa taasisi za serikali.

Ushauri huo ulitolewa jana ikiwa siku moja baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwasilisha ripoti za mwaka wa fedha 2021/22 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu, Dar es Salaam juzi.

Ripoti hizo zilionyesha kuwapo madudu yakiwamo matumizi mabaya ya fedha katika taasisi za umma na miradi ya maendeleo, hali inayochangia kuitia serikali hasara na kurudisha nyuma maendeleo.

Kiongozi wa ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, amepongeza mapendekezo ya kuundwa kwa tume ya kuchunguza fedha za 'plea bargaining'. Alisema tume hiyo ikiundwa itapitia malalamiko ya watu wote ambao walilipishwa fedha na DPP kwa mtindo wa kukiri makosa na kulipa fedha hizo serikalini.

Kupitia ukurasa wake wa 'Twitter' jana, Zitto aliandika: "Aprili 13 tukiwa tunachambua taarifa ya CAG kwa mwaka unaoishia Juni 2020, tulitoa mapendekezo ya kuundwa kwa tume ya kuchunguza uporaji kupitia plea bargain. Tunampongeza sana CAG Charles Kichere kwa kulifanyia kazi pendekezo letu.

"Tulisema wote watakaobainika kuwa walionewa warudishiwe fedha zao na rekodi zao za jinai zifutwe. Tunajua watu wengi tu walionewa wakatoa pesa wakalipishwa, watu walitoa michango mingi kununua uhuru wa watu walioonewa."

Alisema ni muhimu pia ikajulikana kuwa fedha zilizokuwa zikilipwa kwa wale waliokosa hazikupaswa kwenda kwa DPP na badala yake zilistahili kwenda Hazina ambako mlipaji angepeswa risiti ya malipo aliyofanya

Mtaalamu wa uchumi, Prof. Samwel Wangwe, alisema matumizi mabaya ya pesa katika taasisi na miradi ya maendeleo ya serikali pamoja na mambo mengine yanatokana na kutokuwapo na mifumo thabiti ya udhibiti, hivyo kusababisha baadhi ya watumishi kutowajibika ipasavyo.

Kutokana na hali hiyo, aliishauri serikali kuongeza nguvu katika mifumo hiyo ili kuwabana watumishi ikiwamo kuwafuatilia namna wanavyofanya kazi zao.

Alisema udhibiti huo pia unaweza kufanyika kwa kuandaa utaratibu wa kupata maoni kutoka kwa wananchi wa kawaida wanaohudumiwa ili kujua utendaji kazi wa watumishi husika.

Aidha, alisema serikali inatapaswa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuangalia pesa inayotumika kuendesha miradi kama inaendana na thamani ya miradi yenyewe.

"Ni mambo yanayopaswa kufanyika mara kwa mara bila kumsubiri mkaguzi mkuu, yakifanywa mapema ni rahisi kudhibiti upigwaji kuliko yakifanyika mara moja au mbili kwa mwaka," alisema Wangwe.

Kuhusu maagizo ya Rais kufungwa mashirika ya umma yanayoonekana kuwa mzigo, serikali Prof. Wangwe alisema ni vyema yakafanyiwa uchunguzi kwanza ili ionekane tatizo hasa liko wapi. Alisema kama tatizo litaonekana liko kwa watu basi wawajibishwe na kuwekwa wengine wenye weledi na kama yataonekana yamepitwa na wakati yabinafsishwe.

Ofisa Mkuu Mtendaji wa Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema kuna haja ya kuzipa nguvu taasisi zinazokemea matumizi mabaya ya fedha za umma kama vile TAKUKURU, Bunge, vyama vya upinzani na vyombo vya habari.

"Vyombo hivi vina uwezo wa kufanya makubwa isipokuwa kuna mahali vinabanwa. Vipewe nguvu na uhuru wa kukemea suala hili, visiminywe na katika hili kama Katiba ya nchi ikitumika vizuri kila kitu kitakwenda sawa," alisema Dk. Olomi.

Dk. Donath Olomi alisema ni wakati wa serikali kuandaa sera na utaratibu mzuri wa kimfumo zitakazoongoza uwapo wa mashirika ya umma, ili yaanzishwe pale kunapokuwa na ulazima badala yake sekta binafsi zifanye kazi hizo.

"Kitu kinachoweza kufanywa na sekta binafsi hakuna haja ya kufanywa na serikali kwa sababu ina mambo mengi ya kufanya. Kusipokuwa na sera na miongozo, unaweza kufunga mashirika, akaja kiongozi mwingine akayafufua," alisema.

Aidha, aliishauri serikali kuipa kazi kampuni iliyopo nje ya nchi ya kuzimamia mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Bandari ili ishabihiane kwa kuwa tatizo hilo linatokana na kutokuwapo na uwazi, uwajibikaji na usimamizi mzuri kuanzia bodi hadi wizara husika.

Kauli hiyo iliungwa mkono na Mhadhiri wa Chuo Kikuu Mzumbe, Ndaki ya Dar es Salaam, Dk. Godbertha Kinyondo, aliyeishauri serikali kuboresha mitandao ya kiutendaji katika taasisi hizo ili kusimamia ipasavyo uwazi na kuondoa sintofahamu ya kiutendaji.

Alisema taasisi hizo zinapaswa kuweka pembeni ushindani na kufanya kazi kwa ushirikiano kwa kuwa zote zina lengo la kuongeza mapato, kukuza uchumi na kuiletea nchi maendeleo.

## Makandarasi wapongeza agizo la Rais Samia

**Na Maulid Mmbaga**

MAKANDARASI wamepongeza kauli na maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kulipatia ufumbuzi tatizo la kucheleweshwa kwa malipo ya makandarasi wanaotekeleza miradi mbalimbali.

Juzi, Ikulu jijini Dar es Salaam, wakati akipokea ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka 2021/22, Rais Samia aliwaagiza makatibu wakuu na maofisa masuhuli kuhakikisha wanalipa fedha za makandarasi kwa wakati.

Pia aliwataka kujiepusha na ucheleweshaji unaosababisha riba na kwamba suala hilo linawarudisha nyuma makandarasi na kuchelewesha miradi.

Ripoti ya CAG ilionyesha kuwa katika mwaka huo wa fedha, Sh. milioni 418 zilitumika kulipa makandarasi riba kutokana na kucheleweshwa kwa malipo.

Akizungumza na Nipashe jana, msimamizi wa mradi wa usambazaji wa umeme vijijini mkoani Njombe unaotekelezwa chini ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Nicholas Lazaro, alisema wameipokea vizuri kauli hiyo ya Rais Samia.

"Tatizo la baadhi ya makandarasi kucheleweshewa malipo endapo litafanyiwa kazi, litasaidia miradi kutekelezwa kwa ubora na kukamilika kwa wakati kulingana na mikataba husika.

"Makandarasi wengi wanafeli kumaliza miradi kwa wakati na kwa ubora kutokana na kucheleweshewa fedha. Endapo suala hilo litashughulikiwa, litasaidia kwa kiasi kikubwa miradi kukamilika kwa wakati," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mpito wa Umoja wa Makandarasi Tanzania (TUCASA), Samuel Marwa, aliiomba serikali kuangalia upya uwezekano wa kuwa na kanuni zitakazotoa mwongozo kwa makandarasi kulipwa kwa wakati. Alisema hiyo itawezesha kutekelezwa kwa ufanisi miradi waliyopewa kwa sababu baadhi hushindwa kutokana na kucheleshewa malipo.

**ALICHOSEMA RAIS**

Akizungumzia suala hilo, Rais alisema kuna watu wizarani wanachelewesha malipo ya makandarasi kwa makusudi ili walipe kwa riba kwa sababu katika malipo hayo na wao wananufaika. Alisema endapo makandarasi watalipwa kwa wakati, watatekeleza kazi hizo kwa ufanisi.

"Makatibu wakuu na maofisa masuhuli tutakabana koo kwenye hili. Haipendezi kila ripoti ya CAG kuna malipo ya riba. Imagine (fikiria) Sh. milioni 418 ni riba, haiwezekani malipo hayana tija. Hizi fedha tungezipeleka kwenye umeme tungepeleka huduma kwa watu wangapi?

"Tunahangaika kutafuta pesa ya umeme huku tunalipa malipo na riba. Mijitu ipo tu haina uzalendo, haijali. Wanazalisha riba wanalipa wapate na cha kwao," alisema.

Aidha, kwenye suala la malipo ya riba, aliwaelekeza wanaosimamia kuwa wakali, akisisitiza kuwa hakuna sababu ya kulipa riba.

"Juzi nilisema makandarasi wadogo wa ndani sheria ya serikali inasema malipo yatafanywa ndani ya siku 90. Mkandarasi anamaliza kazi yake analeta 'certificate' yake mapema anasubiri umlipe aendelee na kazi yake. Unachelewesha kwa sababu unalindo la siku 90, asipofanya kazi unamgeukia unaenda kusema umeshindwa kufanya kazi. "...ukimlipa mkandarasi mdogo na yeye huyu ndio anayeenda Kariakoo, ndio anakwenda kununua bia, saruji mzunguko wa fedha unakuwapo. Lakini serikali mnabana nina siku 90, huyu mnamweka na njaa, kazi inachelewa. Hii siyo sawa, naomba sana wasimamizi mlisimamie hilo," alisisitiza.

# PIC yabaini tatizo ujenzi barabara mwendokasi TAZARA

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PIC), imebaini tatizo kwenye ujenzi wa barabara ya mwendo wa haraka (BRT), awamu ya tatu eneo la daraja la juu la Mfugale, katika makutano ya Barabara ya Nyerere na Mandela (TAZARA) jijini Dar es Salaam.

Tatizo hilo ni namna barabara hiyo ilivyopitishwa katika eneo hilo na kupata wasiwasi kwamba ipo hatari ikaja kusababisha foleni kubwa baada ya kuanza kutumika na kuondoa maana ya kujengwa kwake.

"Lengo kubwa la kujenga barabara hii ni kusaidia kupunguza foleni na kurahisisha usafiri, lakini kwa namna ilivyopitishwa katika eneo hili, tunaona kwamba itakuja kusababisha foleni kubwa hasa kwa sababu malori nayo yanatumia njia hii ya chini kwenda bandarini na kama itatokea hilo, itakuwa haina maana ya kujenga barabara ya mwendokasi huku," alisema Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka.

"Hivyo tumeshauri Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) kuangalia uwezekano wa kutatua hilo kabla ya mradi wake kumalizika na kuanza kutumika ifikapo mwaka kesho. Barabara hii inapitisha malori mengi kwenda bandarini na yanapita chini, sasa na mwendokasi nao ukipita chini itakuja kusababisha foleni kubwa mno na itakuwa haina maana tena."

Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Rogatus Mativila, alisema wamepokea ushauri uliotolewa kamati hiyo na wataufanyia kazi.

"Tutafanyia kazi ushauri huu na tunaweza kuinyanyua juu zaidi. Lakini tunafikiria kujenga barabara ya juu katika makutano ya barabara pale Buguruni.

Tatizo jingine ambalo kamati hiyo ilibaini ni kuwapo kwa baadhi ya taasisi za umma zinazokwamisha mradi huo.

Alisema mpaka sasa mradi huo ulitakiwa uwe umefikia asilimia 15, lakini uko nyuma kwa asilimia 10 na sababu inatokana na kukutana na vikwazo kutoka baadhi ya taasisi za umma. "Kuna taasisi ya umma baada ya mradi kuanza iliweka vikwazo, yaani mradi umeshaanza na mkandarasi ameanza kujenga karakana, ikasema iondolewe, akaenda tena eneo jingine nako akaambiwa aondoe bila kujali muda wote huo fedha ya serikali inatumika, hii ni mbaya sana," alisema Kaboyoka.

"Ombi langu kwa taasisi hizi za umma ziache kukwamisha miradi kwa sababu kufanya hivyo ni kupoteza fedha za umma na pia kunaichelewesha isimalizike kwa muda unaokuwa umepangwa. Ikumbukwe kwamba mradi huu unajengwa kwa mkopo."

Ujenzi wa BRT awamu ya tatu mkataba wake ulisainiwa Machi 17, mwaka jana na kuanza rasmi ujenzi Agosti mwaka jana, ukitarajiwa kukamilika baada ya miezi 20, na kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 230.

# Puma Energy yadhamiria kuwekeza miundombinu ya viwanja vya ndege

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Puma Energy imesema imedhamiria kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ya viwanja vya ndege nchini Tanzania ili kusaidia ukuaji wa muda mrefu na uendeshaji katika mazingira salama.

Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Fatma Abdallah, alisema jana kuwa Puma Energy inawekeza katika ujenzi wa bomba jipya la maji ya kusaidia kukabiliana na majanga ya moto katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, na inapanga kuweka mifumo ya kisasa ya kidijitali katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume mjini Zanzibar ili kupunguza ucheleweshaji na kuimarisha viwango vya huduma.

Alisema: "Duniani kote, huduma za Puma Energy katika sekta ya anga zinaaminiwa kwa ufanisi na kwa usalama na mashirika ya ndege. Utoaji huduma wa kampuni ya Puma Energy kwenye viwanja vya ndege nchini Tanzania umevifanya kuwa miongoni mwa viwanja vya kisasa, salama na vya kutegemewa barani Afrika."

Fatma alisema kuwa sekta ya usafiri wa anga ya Tanzania bara na Zanzibar inaonyesha dalili za kuimarika huku kiasi cha matumizi ya mafuta ya anga kikiongezeka baada ya changamoto ya miaka miwili iliyosababishwa na janga la COVID-19.

Kwa muujibu wa kampuni hiyo inayofanya kazi katika viwanja vinane vya ndege nchini Tanzania bara, kiasi cha matumizi ya mafuta ya ndege kimeongezeka kwa asilimia 45 mwaka 2022 nchini Tanzania ikikaribia viwango vya kabla ya COVID-19. Kwa Zanzibar, matumizi yameongezeka kwa asilimia 43 katika kipindi hicho cha mwaka na kuvuka matumizi ya mwaka 2019.

"Kurejea kwa viwango vya juu vya matumizi ya mafuta ya ndege ni kielelezo kinachodhihirisha kuwa sekta ya utalii imeanza kufanya vizuri nchini kwa upande wa Tanzania bara na Zanzibar, pia kunatoa taswira ya kuongezeka kwa hali ya kuwa na ari ya uwekezaji miongoni mwa wadau wa sekta hiyo," alisema Fatma.

"Utalii unachangia sana ukuaji wa uchumi wa Tanzania na uwekezaji wetu wa sasa na uliopangwa katika miundombinu na vifaa vya kisasa vya kujaza mafuta katika viwanja vyote vya ndege nchini Tanzania umekuwa muhimu sana tunaposhirikiana kwa karibu na mamlaka husika kusaidia mashirika ya ndege ya ndani na kushawishi mashirika ya ndege ya kimataifa kuongeza safari za Tanzania," alisema.


BONITE BOTTLERS LIMITED

Advertisements of Employment

1. **Mechanical Technician**
   **Qualification:**
   - Applicant should be a holder of VETA level III in Mechanical Engineering from a recognised Institution.

   **Key skills & Abilities:**
   - Ability to maintain and troubleshooting all the mechanical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation and to ensure smooth running of the line and service equipment by close communication with other staff.
   - Ability to operate machines as directed and to ensure they are running smoothly, efficiently and kept clean as required.
   - Able to work independently with minimum supervision
   - Self motivated, flexible person and a good team player.
   - Compliance to safety requirement at work place

2. **Electrical Technician**
   **Qualification:**
   - Applicant should be a holder of VETA level III in Electrical Engineering from a recognised Institution.

**Key skills & Abilities:**
- Ability to maintain all the electrical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation, and to ensure the smooth running of the line and service equipment by close communication with other staff.
- Ability to operate the machines as directed and to ensure they are running smoothly and efficiently as required and kept clean as required.
- Ability to ensure the correct electrical functioning of electrically operated equipments on the premises.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated, flexible person and a good team player.
- Compliance to safety requirement at work place

√ **Experience:** Six months and above in Mechanical/Electrical field
√ **Location:** Moshi.

**Mode of Application:**
All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to the undersigned, to reach him not later than 11/04/2023.

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI.**

217346202



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ANAWATANGAZIA WATU WOTE WALIOPATIWA VIWANJA ENEO LA NYAFULA NA SANGABUYE NA HAWAJAKAMILISHA MALIPO YAO KUWA ANATOA MUDA WA SIKU 14 KUANZIA TAREHE **29 MACHI 2023** HADI **11 APRILI 2023** KUKAMILISHA MALIPO YA VIWANJA HIVYO.

KWAMBA KWA YEYOTE AMBAE ATAKUWA HAJAKAMILISHA MALIPO NDANI YA SIKU 14 ATANYANG`ANYWA KIWANJA NA KITAUZWA KWA MTU MWINGINE BILA KUPEWA TAARIFA KWA KUWA MUDA WA KULIPIA KWA WATEJA WOTE UMESHAKWISHA KWA MUJIBU WA ANKARA (INVOICE) ULIYOJAZA WAKATI ULIPOGAWIWA KIWANJA.

TANGAZO LIMETOLEWA NA:
ENG MODEST J. APOLINARY
MKURUGENZI WA HALMASHAURI
MANISPAA YA ILEMELA

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza. Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,Tovuti: www.ilemelamc.go.tz

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Hatua zichukuliwe dhidi ya madudu katika ripoti CAG*

**MDHIBITI** na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, juzi aliwasilisha Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za mwaka 2021/22 kwa Rais Samia Suluhu Hassan Ikulu jijini Dar es Salaam. Katika ripoti hiyo, kuna mambo mengi yaliyoibuliwa kuonyesha matatizo makubwa ya kimfumo na kiutendaji katika serikali na taasisi zake.

Miongoni mwa mambo yaliyoibuliwa katika ripoti hiyo ni mifumo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na ile ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokusomana hatua ambayo inatoa mwanya wa kuvuja kwa mapato. Kama alivyosema Rais Samia baada ya kupokea ripoti hiyo, bandari ndilo lango kuu la kuipatia serikali mapato, hivyo kunapokuwa na kasoro yoyote, kuna uwezekano wa makusanyo ya serikali kupungua.

Aidha, CAG Kichere alibainisha kuwa kuna ubadhirifu wa hali ya juu wa fedha za umma kwenye miradi mbalimbali hususani katika mamlaka za serikali za mitaa, mikopo ya halmashauri kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu. Sambamba na madudu hayo, miradi ya maji katika baadhi ya maeneo haifanyi kazi kwa maana ya kutoa huduma kutokana na visima kadhaa kutotoa maji.

Pamoja na yote hayo, CAG pia alibainisha kuwa kuna mikataba ya ujenzi wa miradi ya kimkakati ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na bwawa la Mwalimu Nyerere ina kasoro, hivyo kusababisha ucheleweshaji katika kukamilika na hatimaye kuisababishia serikali hasara kwa kulipa fedha zaidi ya zile zilizokusudia.

Jambo lingine aliloligusia ni kuwapo kwa mashirika ya umma ambayo hayajiendeshi kwa faida. Hatua hiyo imeifanya serikali kutoa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa mashirika hayo huku Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ikielezwa kwa mara nyingine kuwa lina mtaji hasi licha ya serikali kuwekeza kwa kiasi kikubwa ikiwamo kununua ndege mpya za abiria na kuliwezesha kimtaji.

Kutokana na kuibuliwa kwa madudu hayo, kama ambavyo imekuwa ikitokea kila mwaka ripoti za CAG zinapotolewa, Rais Samia aliweka bayana kwamba kuna umuhimu wa kuchukua hatua zikiwamo kuwawajibisha wale wanaohusika na dosari hizo. Pia Rais aliagiza uchambuzi wa kina ufanyike kwa mashirika ya umma na hatimaye kuyafuta yale ambayo yamekuwa mzigo kwa serikali.

Kwa ujumla, kila mwaka ripoti za CAG zinapotolewa kumekuwa kukiibuliwa madudu jambo ambalo linaonyesha kuwa hakuna hatua kali zinazochukuliwa dhidi ya wanaohusika na mambo hayo. Wakati umefika sasa wa kuchukua hatua ili kukomesha baadhi ya mambo ambayo yamekuwa yakijirudia na hatimaye kufikia kuwapo kwa taarifa zinazoonyesha mambo yanakwenda sawa katika serikali na taasisi zake.

Watendaji wakuu wa mashirika na taasisi pamoja na wale wa halmashauri ambao wameguswa na taarifa mbaya kwenye ripoti ya CAG wanatakiwa kuwajibishwa kama alivyosema Rais. Ni dhahiri kwamba iwapo watu hao watachukuliwa hatua, wengine waliopewa dhamana na watakaopewa siku zijazo, watakuwa makini katika utendaji wao kwa kuwa watakuwa wanajua fika kwamba wakiboronga lazima watatumbuliwa.

Katika eneo la bandari kwa mfano, hatua zinatakiwa kuchukuliwa haraka ili kuhakikisha mifumo inayodaiwa kuwa na kasoro inarekebishwa na hatimaye kuiwezesha serikali kukusanya mapato kwa ufanisi. Haiingii akilini kuona sehemu ambayo ni tegemeo kubwa katika kuiingizia serikali unafanyiwa hujuma kwa kuchezea mifumo halafu wahusika wanaendelea kuachwa tu.

Ni imani kwamba kama hatua stahiki zitachukuliwa kwa kufanyia kazi yale yote ambayo yamependekezwa na CAG pamoja na maagizo ya Rais, kutakuwa na nidhamu kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hatimaye wananchi kupata kile wanachostahili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# *Miaka miwili bila JPM, miradi aliyoacha inaendelezwa kwa tija*

Na Sabato Kasika

**LEO** wiki mbili tangu kuanza safari kuelekea mwaka wa tatu, kupita wa kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17 mwaka 2021, akiwa na ndoto ya kuhakikisha Tanzania inajitegemea kiuchumi.

Rais Dk. Magufuli aliondoka akiwa ameacha alama, kutokana na miradi mbalimbali ya maendeleo aliyokuwa ameianzisha, ikiwamo bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, reli ya kisasa na mingine mingi.

Kwa ujumla ni kwamba, alichokifanya katika nchi hii, kinaonekana ikiwamo kuimarisha miundombinu ya bararaba, huku akiwataka wasaidizi wake kuwahudumia wananchi na kutatua kero zinazowakabili.

Jitihada zake, pia zilizaa matunda ya kuwapo kwa barabara za juu katika jiji la Dar es Salaam na kusaidia kupunguza foleni za magari ambazo zilikuwa zikilalamikiwa kuchangia kudidimiza uchumi.

Pia, aliamini katika juhudi za kufanya kazi kwa nguvu, juhudi na maarifa, inawezekana na kuishia watu kujiletea maendeleo. Akazuia vijana kushinda vijiweni badala yake wafanye kazi ili kujiletea maendeleo.

Ikiwa ni wiki hizi mbili tangu kumalizika kwa miaka miwili ya kifo chake, pia miaka miwili ya mrithi wake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni vyema kutambua juhudi za viongozi hao katika kuleta maendeleo ya nchi. Rais Dk. Magufuli hayupo tena, lakini bahati nzuri ni kwamba, mrithi wake naye anapita katika nyayo zile zile, kwa kuendeleza na kusimamia miradi alionzisha mtangulizi wake ili kuhakikisha anakamilika.

Miongoni mwa miradi hiyo ni, bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa barabara za juu jijini Dar es Salaam, za mabasi ya mwendokasi na mingine katika maeneo mbalimbali nchini.

Rais Dk. Samia amekuwa akisisitiza kuwa serikali ya awamu ya sita inaendelea kukamilisha miradi yote ya maendeleo iliyoanza wakati wa serikali ya awamu tano na kwamba miradi mingi imeanza kukamilika kwa hatua mbalimbali.

Mkazo wa Rais kwa wananchi, ni kuwataka kuhakikisha wanatunza miundombinu inayojengwa na serikali, ikiwamo barabara na madaraja, ili idumu na kuchangia maendeleo ya kitaifa.

Anaweka wazi kuwa serikali haitawafumbia macho watendaji 'wanaopiga dili' katika miradi ya maendeleo na kusababisha makandarasi wasiokuwa na sifa kupata kazi au kupitisha miradi iliyo chini ya viwango vinavyotakiwa.

Ninadhani kwamba, kila mmoja wetu anahusika katika kuhakikisha miradi ya maendeleo inaimarika kwa watendaji kuisimamia vizuri, pia wananchi kuwa tayari kutoa kwa vyombo vya dola wanapoona miradi inahujumiwa.

Pamoja na hayo, wakaguzi wa miradi hawana budi kujiweka mbali na rushwa kutoka kwa makandarasi katika harakati za hatua za kuhitaji kupitishwa miradi mibovu, inayoweza kuliingiza taifa kwenye hasara zisizotarajiwa.

Kimsingi ni kwamba, iwapo kila mmoja wetu atafanya sehemu yake kwa uaminifu, itakuwa rahisi kwa serikali kufikia malengo ambayo imejiwekea kwa ajili ya maendeleo ya taifa na watu wake.

Maana yake ni kwamba, hakupaswi kuwapo wachakachuaji miradi, wala wanaoiba miundombinu ya miradi yenyewe, kwani kwa hatua hiyo, itakuwa rahisi kwa taifa kusonga mbele kimaendeleo na kiuchumi.

Kile ambacho Rais amekuwa akitamani, ni kuona utekelezaji miradi ya maendeleo unaofanywa katika maeneo mbalimbali nchini, unakwenda sambamba na ukusanyaji wa mapato, ili kukuza uchumi wa nchi.

Ukweli ni kwamba, Rais anachukizwa na rushwa, ubadhirifu wa fedha, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwani vitendo hivyo vinaweza vikavuruga jitihada za serikali za kuinua uchumi wa nchi.

## Kamati yataka serikali Kenya kufikia maridhiano na wapinzani

**Na Beatrice Shayo**

KAMATI ya Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania imeiomba serikali ya Kenya kukaa meza moja na wanasiasa ili kupata maridhiano ya kweli na yenye amani badala ya kusababisha vurugu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Shekhe Alhad Mussa Salum, alisema vurugu hizo zinasababisha changamoto mbalimbali ikiwamo nyumba za ibada kuchomwa moto, hivyo ni muhimu wakatafuta maridhiano kwa pamoja.

Alisema maridhiano hayo yatazaa utulivu, amani na kuondoa vurugu zinazoendelea ndani ya nchi hiyo ambazo zinaweza kusababisha hasara kubwa.

"Serikali ya Kenya na wanasiasa watangulize uzalendo na kufanya maridhiano ili wafanye siasa ya amani na yenye kuleta tija kwa nchi yao," alisema Shekhe Salum.

Shekhe Salum alitolea mfano kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan wa kuleta maridhiano ya kweli kwa wanasiasa hadi sasa nchi inafanyika siasa za pamoja zenye maendeleo.

"Wanasiasa wa nchini Kenya wachukue mfano wa Rais Dk.Samia ya kukaa pamoja na wanasiasa wote na kuleta maridhiano ya kweli nchini," alisema.

Aidha, alisema katika kipindi hiki cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani Waislamu wanatakiwa kufunga kwa imani na kuiombea heri nchi yao na familia zao.

"Kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ndicho kipindi Waislamu wanakuwa karibu na Mwenyezi Mungu hivyo watumie bahati hiyo kwa kuomba heri ya nchi na familia zao," alisema.

Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Askofu Dk. Gabriel Maasa, alisema amani ni muhimu kuliko cheo kila mmoja atizame suala la amani na maslahi ya taifa ni bora kuliko maslahi binafsi.

"Maslahi binafsi yasiharibu amani ya taifa badala ya vurugu na maandamano wakae meza moja ya mazungumzo ili kuondoa changamoto zilizojitokeza na si kuvuruga amani ya nchi," alisema Maasa.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, akizungumza na wananchi baada ya kushiriki kufanya usafi wa mazingira katika zahanati ya kijiji cha Ruponda, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aliyeshtakiwa kuua mke kwa kumchoma moto aomba mahakama imwachie huru

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwonga (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, ameomba Mahakama Kuu imuachie huru kwa sababu hadi sasa hakuna ushahidi wa kutosha wa kumshtaki.

Luwonga aliwasilisha ombi hilo jana mbele ya Jaji Obadia Bwegoge kupitia kwa wakili wake, Mohamed Majaliwa na kuiomba mahakama kesi ya mauaji namba 5 ya mwaka 2022 iliyopo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa ina upungufu kisheria.

Majaliwa alidai kuwa mteja wake anashtakiwa kwa kosa la mauaji mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Rhoda Ngimilanga wa Mahakama ya Kisutu, alidai shauri hilo linaonekana jipya, lakini kiuhalisia sio jipya kwa sababu kesi ya mauaji namba 4, 2019 dhidi ya mshtakiwa ilishaisha.

Alidai kuwa mashtaka yaliyokuwapo kwenye hati hiyo yalipita katika hatua zote za kisheria, Oktoba 24, 2022 kesi iliitwa kwa ajili ya kusikilizwa na upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi wanne.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mwasiti Ally, alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Ruboroga wa Mahakama ya Kisutu kuwa kesi ililetwa kwa ajili ya kusikilizwa, lakini Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), hana nia ya kuendelea na mashtaka dhidi ya mshtakiwa.

Majaliwa alidai kutokana na kuomba kuondolewa kwa kesi hiyo, Hakimu Ruboroga alimwachia Luwonga, lakini cha kushangaza mshtakiwa alikamatwa tena na askari na baada ya saa chache alipandishwa tena kizimbani na kusomewa mashtaka yale yale.

"Chakushangaza Mwasiti huyo huyo aliyeomba kesi namba 4, 2019 kuondolewa ndiyo aliyemsomea mashtaka mapya mshtakiwa na kudai upelelezi bado haujakamilika, kwa hiyo mahakama ikatoa amri ya Luwonga kurudishwa rumande

"Hadi sasa hivi jalada lililokuwa mbele yako linaonesha upelelezi bado haujakamilika ni rai yetu kwamba mashtaka haya mapya ni batili mbele yako kwa sababu yanakiuka sheria," alidai Majaliwa. Alidai sheria imetoa utaratibu kama mtu akiachiwa na serikali ikataka kumshtaki tena basi ni lazima kuwapo na ushahidi wa kutosha na usikilizwaji wake uanze mara moja, lakini katika kesi hiyo hilo halikuzingatiwa.

Ukijibu hoja hizo, upande wa mashtaka ulidai kuwa mahakama hiyo imefungwa mikono kutoa amri kwenye amri ambazo hazijafika mwisho.

Katika hoja ya kuachiwa kwa mshtakiwa, upande huo ulidai kuwa hoja hiyo inakizana na matakwa ya kisheria na pia taratibu za kisheria bado hazijakamilika kwa sababu kesi bado haijafika Mahakama Kuu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Baada ya Jaji kusikilizwa hoja za pande zote mbili ameahirisha maombi hayo hadi Aprili 18, 2023 kwa ajili ya uamuzi. Pia mshtakiwa anatetewa na Zidadi Mikidadi na Fatuma Abdul.

Luwonga amefungua maombi Mahakama Kuu ili wapate maelezo ya uhalali wa kesi namba 5, 2022 ya mauaji baada ya kesi ya awali ya kufutwa na kufunguliwa upya.

Katika kesi hiyo ya mauaji, mshtakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni alimuua Naomi Marijani.

Anadaiwa kumuua mke wake Naomi kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa na kuchukua majivu ya marehemu na kwenda kuyafukia shambani kwake.

**KABWELA** — **Na Fadhili Mohammed**





# Mgogoro wanyafakazi, kiwanda wapatiwa ufumbuzi

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

SIKU mbili baada ya kuibuka mgogoro wa wafanyakazi 500 wa kiwanda cha kutengeneza chuma cha Lodhia dhidi ya mwajiri wao wakigomea kufanya kazi ili kushinikiza nyongeza ya mshahara hatimaye serikali imeupatia ufumbuzi.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, aliumaliza rasmi mgogoro huo na kuwataka wafanyakazi hao kurudi kuendelea na kazi kutokana na kufikiwa makubaliano na pande zote mbili.

"Tumeshazungumzia kero zenu na waajiri wenu na tayari wamekubali kuongeza mshahara kutoka kima cha chini walichokuwa wakiwalipa ikiwa ni pamoja na kuwapatia vifaa vya kazi mnapokuwa kazini," alisema Mtahegerwa.

Aidha, Mtahengerwa, aliwataka wafanyakazi hao kufanya kazi kwa uaminifu na kuacha tabia za wizi kiwandani hapo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Lodhia, Harun Lodhia, alisema amependisha mshahara kutoka Sh. 150,000 kwa kima cha chini hadi Sh. 180,000.

"Mbali na mshahara huo kuna pesa ya chakula nayo imepanda kutoka shilingi 1,800 hadi 2,000 pamoja na pesa ya maziwa nayo imeongezeka kutoka shilingi 800 hadi 1,000 kwa kila mfanyakazi.

"Sasa kwa kuwa sisi Lodhia tumekubaliana na shinikizo lenu na ninyi fanyeni kazi kwa bidii ili mpande madaraja, kwa kuwa kila mnapopanda madaraja na mshahara unapanda."

Nje ya kiwanda hicho, baadhi ya wafanyakazi akiwamo Ally Tete, alisema kilichowasukuma kufanya mgomo huo ilikuwa pia ni kupinga kufanyishwa kazi ngumu, huku malipo yake yakiwa kidogo.

Mfanyakazi mwingine, ambaye hakutaka jina lake kutajwa, alisema: "ukiugua, ukienda kutibiwa hospitali ndogo, huwa hawatambui na huwa tunakatwa pesa, kwa sababu wanataka cheti chenye ithibati ya hospitali kubwa. Na wakati huo huo, hatulipiwi matibabu, zaidi ya kukatwa na mishahara yetu."




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe (watatu kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mtibwa Sugar, Seif Ali Seif (wa pili kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Siemens Ukanda wa Afrika, Sabine Dall'omo (wa tatu kulia) kwa pamoja wakikata utepe kufungua rasmi darasa la TEHAMA katika Shule ya Msingi Kiwandani, lililokarabatiwa kwa ushirikiano wa Mtibwa Sugar na Siemens, wilayani Mvomero, mkoani Morogoro jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Madizini, Goodluck Mugeta (kushoto), Ofisa Elimu wa Wilaya hiyo, Bruno Sangwa (wa pili kulia) na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Philemon Sokime. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Pinda aongoza harambee ujenzi Kanisa KKKT

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amechangisha zaidi ya Sh. milioni 43 kwa ajili ya ujenzi wa kanisa jipya la kisasa la Usharika wa Ungalimited wa Dayosisi ya Kaskazini Kati ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Katika harambee hiyo ambayo yeye alitoa Sh. milioni 10 aliahidi kumuomba Rais Samia Suluhu Hassan na marafiki zake kuchangia ujenzi huo unaotarajiwa kutumia zaidi ya Sh. milioni 500.

Akizungumza katika halfa ya ukusanyaji wa fedha hizo jana, Pinda alisema alipopata barua ya mwaliko wa kuwa mgeni rasmi katika harambee hiyo, alilazimika kutii haraka kwa kuwa anajua anayekwenda kumtumikia ni Mungu atupaye kila kitu.

Tangu kuanza kwa harambee ya kuchangia mradi huo wa ujenzi, Sh. milioni 168 hadi sasa zimekusanywa, ambapo fedha taslimu ni zaidi ya Sh. milioni 84, huku ahadi ikiwa ni zaidi ya Sh. milioni 83.

Katika nasaha zake kabla ya kuchangisha fedha hizo, Pinda, aliwataka waumini wa KKKT, kutunza mazingira ili kurejesha uoto wa asili na nchi kuendelea kuwa na mazingira mazuri.

Jengo jipya la kanisa hilo litakuwa na uwezo wa kuchukua watu 1,500 hadi 2,000 kwa wakati mmoja.

Awali Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Godson Abel, aliwasihi Wakristo kukemea vitendo vya ukatili, ushoga na ulawiti, akisisitiza kuwa ni chukizo mbele za Mungu.

"Ushoga na ukatili ni chukizo kwa Mungu tunapiga vita mambo haya maana yanamkasirisha Mungu, vitendo hivi viovu tunasikia habari ya watoto kulawitiwa hii ni mbaya na tunaikemea kwa nguvu zote,"alisema.

Aidha, Dk. Abel, alisema ushiriki wa Pinda katika harambee hiyo ni baraka kubwa katika Usharika wa Ungalimited.

# RC awaagiza TEMESA kuboresha huduma

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella amewashauri Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) kuboresha huduma, kuzitoa kwa gharama nafuu, ili wadau wa serikali, taasisi na idara zake waifanye kuwa kimbilio la kwanza katika matengenezo ya magari.

Mongella aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Arusha, wakati wa ufunguzi wa kikao cha wakala huyo na wadau wake ambao ni idara, taasisi na wakala za serikali.

Alisema huduma zikiboreshwa hakuna mdau atakayekimbilia mtaani, badala yake atakimbilia TEMESA ambao kimsingi walianzishwa ili wadau serikalini waitumie.

"Lakini miaka ya hapo nyuma kulikuwa na chagamoto ya utoaji huduma zao, tofauti na sasa kuna maboresho makubwa lakini endeleeni kuboresha ili tuifanye kimbilio letu la kwanza, maana ukipata huduma bora hutakimbilia mtaani," alisema.

Aidha, aliomba wadau wa TEMESA zikiwamo idara, taasisi na wakala za serikali kumuunga mkono wakala huyo ili nayo iendelee kutoa huduma bora.

"Kama tupo kwenye soko tunahitaji huduma nzuri zilizopo katika soko lakini ziwe gharama ambazo mdau naye anazimudu, ni lazima tubadilike tuone TEMESA tofauti na ya nyuma," alisema.


Alisisitiza fursa za TEMESA ni kubwa sababu katika majengo ya serikali mengi kuna ujenzi wa majengo na kazi mbalimbali zinaendelea, hivyo huduma zikiwa nzuri na kazi watapata nyingi. Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi Umeme (TEMESA), Lazaro Kilahala, alisema wakala huyo ni taasisi wezeshi yenye kutoa huduma kwa serikali katika kuleta ufanisi zaidi.

Alisema TEMESA awali ilikuwa haifanyi vema katika matengenezo ya magari ikiwamo gharama kubwa ya ufundi lakini sasa hivi imeanza kutumia utaratibu mpya wa kupunguza muda wa uagizaji wa vipuri pia kwa kutumia mzabuni.

"Utaratibu huu utamfunga aliyeagiza vifaa kuhakikisha vifaa vinavyoagizwa sio feki, bali viwe sahihi ili kuondokana na lawama na pia tunatoa huduma kwa bei stahiki ya serikali," alisema. Pia aliishukuru serikali kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kukarabati miundombinu yake kwa ajili ya kuhakikisha huduma zao zinakuwa bora na kununua vifaa vya kisasa.

Alitoa mfano kwa Mkoa wa Arusha kuna ukarabati mkubwa wa karakana unaoendelea ili uendane na uhalisia wa utoaji huduma.

Kilahala alisema: "Safari ya mabadiliko ya TEMESA imeshaanza tunaomba tupate maoni yenu ili kuiboresha ambayo mnatamani iwe pia tunamshukuru Rais Samia Hassan Suluhu, kwa kuimarisha TEMESA yenye tija na fanaka zaidi."





# Waliokwenda kutoa elimu ya Marburg visiwani warejea

**Na Titus Mwombeki,** BUKOBA

MELI ya matibabu ya Jubilee Hope iliyobeba wataalamu wa afya kwenda katika visiwa vilivyoko Ziwa Victoria kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na ugonjwa wa Marburg imerejea katika Bandari ya Bukoba.

Akizungumza baada ya meli hiyo kutia nanga katika Bandari ya Bukoba, Juma Rashidi ambaye ni nahodha alisema kuwa walianza safari hiyo wakitokea mkoani Mwanza Machi 24, mwaka huu, wakiambatana na wataalamu hao na walitembelea visiwa vitano na kutoa elimu juu ya ugonjwa huo.

Alivitaja visiwa hivyo ni Rushonga, Nyaburo, Makibwa, Kelebe pamoja na Goziba.

Kiongozi wa msafara huo, Dk. Uzia Mohamed, alisema katika safari hiyo walifanikiwa kutoa elimu kuhusu namna ya kujikinga na ugonjwa huo, huku akiwasisitiza wananchi hao kuendelea kuchukua tahadhari juu ya magonjwa ya mlipuko.

Naye Magandu Godwin mkazi wa Kisiwa cha Kelebe, aliishukuru serikali kwa kufanya juhudi za haraka kuwapelekea wataalamu wa afya, huku akiiomba serikali kupeleka huduma ya kupima joto mwili kwa kila mtu atakayeingia na kutoka katika visiwa hivyo.



Mjumbe wa Jumuiya ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Ukanda wa Ziwa Victoria ambaye ni Meya wa Manispaa ya Musoma, William Gumbo, akipanda mti katika kituo cha afya Karume, wilayani Ilemela, mkoani Mwanza juzi, lengo ni kuhakikisha jamii inaendelea kutunza mazingira. Jumuiya hiyo, imelenga kupanda miti milioni moja katika mikoa mbalimbali hapa nchini kwa mwaka huu. Kulia kwake ni mwanafunzi wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Loreto, Rhoidacmmy Sunday. **PICHA: ROSE JACOB**

# Wajasiriamali 1,000 wafunzwa kuhifadhi mazingira

**Na Waandishi Wetu**

WANAWAKE 1,000 wanaojihusisha na ujasiriamali mkoani Mwanza, wamepewa mafunzo ya namna ya kuhifadhi mazingira, matumizi ya nishati ya gesi katika shughuli zao ili kudhibiti ongezeko la hewa ya ukaa nchini.

Wanawake hao ni pamoja na mama lishe ambao wamepewa elimu ya matumizi ya nishati ya gesi ili kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Akizungumza katika mafunzo hayo ya siku moja jijini humo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema wizara hiyo inaendelea kulinda na kuokoa maliasili ikiwa na kuwaepushia wanawake madhara yatokanayo na matumizi ya mkaa na kuni.

"Mwanza ni moja ya mikoa iliyo na eneo kubwa la msitu na imeathiriwa na ukataji mkubwa wa miti, takwimu zimeonyesha zaidi ya asilimia 60 wanatumia mkaa na kuni hii ni hatari kwa ustawi wa mazingira na taifa kwa ujumla,"alisema Mary.

Alisema wakazi wengi katika eneo hilo hususani vijijini, hutegemea kuni kwa kupikia na kupasha joto, hivyo hulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta kuni na miti ya kuchoma mkaa.

Kadhalika mafunzo hayo yaliambatana na shughuli ya ugawaji wa mitungi ya gesi 1,000 iliyotolewa na wadau wa mazingira kwa kushirikiana na waziri huyo pamoja kutolewa kwa Sh.milioni 21 ikiwa ni sehemu ya kuhimiza matumizi ya nishati mbadala.

Naibu Waziri Masanja alitoa majiko 142 ya gesi kwa wanawake na mizinga 100 ya nyuki kwa UWT Wilaya ya Sengerema na kuwataka waangalie sehemu nzuri ya kuiweka mizinga hiyo ili iweze kuzalisha kwa tija na kuinua uchumi wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Oryx Gas Tanzania, Araman Benoite, alisema, katika kukabiliana na uharibu wa mazingira wameamua kushirikiana na Naibu Waziri huyo kugawa mitungi na majiko wakiamini inakwenda kuwa chachu ya kuhamasisha wananchi kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Nao baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo waliomba serikali iangalie upya bei ya kujazia gesi kutokana na gharama ya sasa kuwa kubwa ambapo wanalazimika kutoa Sh. 24,000 hadi Sh.25,000 hali ambayo bado ni tatizo kwa wananchi wenye kipato cha chini.

"Serikali imekuja na suala zuri la kutulinda dhidi ya madhara ya kupikia kuni na mkaa sambamba na kulinda mazingira lakini bei ya kubadilisha hizo nishati mbadala bado siyo rafiki,"alisema Tabia Hassan mkazi wa Kwimba.

**Imeandaliwa na Rose Jacob (Mwanza), Elizaberth Seleman (Sengerema)**

# Serikali yaombwa kutoa elimu ya kilimo kwa vijana

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imeombwa kutoa elimu ya kilimo cha mazao ya biashara na chakula kwa vijana wasiosoma ili kuwawezesha kujiongezea kipato na kuondokana na dhana potofu kwamba kilimo ni adhabu.

Mwenyekiti wa Mzalendo Foundation na Mkulima wa Kata ya Kilago, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Khamis Mgeja, alitoa ombi hilo juzi wakati akizungumza na wakulima na maofisa ugani katika Kijiji cha Lowa.

Alisema kilimo kina fursa nyingi za kuweza kujiajiri vijana vijijini badala ya kuwaacha wakakimbilia mijini, inapaswa wapewe elimu na wawezeshwe pembejeo za kilimo ili wajiajiri katika sekta hiyo ambayo itawasaidia kujikwamua kiuchumi na kuchangia pato la taifa.

Aidha, alisema vijana wengi wanashinda katika michezo ya kubahatisha na kupoteza muda wa kufanya kazi na muda huo wangeutumia shambani wangekuwa wamejikwamua kiuchumi na kuondokana na utegemeze kwenye jamii zao.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Jeremiah Inegeja, alisema kila mwaka wa fedha halmashauri imekuwa ikitenga fedha za ununuzi wa pembejeo za kilimo na kuzigawa bure kwa vijana wakulima wenye uwezo wa kulima kuanzia hekari tano na kuendelea na mazao wanayopata ni mali yao.

Mjumbe wa kamati ya mradi wa elimu ya ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma zilizotolewa kwa ajili ya uboreshaji huduma za kilimo, Charles Kafuku, aliomba serikali kuongeza ajira kwa maofisa ugani ili kuwasaidia wakulima katika masuala ya kupata elimu ya kulima kisasa na kupata mavuno mengi. Emmanuel Andrew ni miongoni mwa wakulima katika kata hiyo aliiomba serikali iwekeze elimu na teknolojia ya kilimo katika vichwa vya vijana ili iweze kuwasaidia kujiajiri.

Chama cha watu wasiona mkoani Shinyanga kinaendelea kutekeleza mradi wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma zilizotolewa kwa ajili ya uboreshaji huduma za kilimo katika kata za Tinde, Didia, Nyandekwa, Igunda, Kinamapula na Kata ya Bukomela kwa ufadhili wa FCS.




Ukurasa 14

Serikali, wadau binafsi wakutana 'kukuna vichwa' kisa halmashauri hazikopesheki




Ukurasa 13

Wasanii hamasisheni kilimo na si matusi na 'kiki' zenu



Ukurasa 12

HIFADHI KITULO NA UPEKEE WAKE


BUFE

IJUMAA MACHI 31, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


UCHUMI

# Bosi COSTECH: Miaka miwili kiserikali, tunaneemeka kwa teknolojia uchumi

• Yabeba tenda kuhudumia nchi kiufundi

**Na Renatha Msungu**

**DODOMA**

HADI sasa serikali iliyo madarakani ikiwa na miaka miwili inaendelea kutumia nyenzo zake za maendeleo, ikiwamo elimu. Hapo Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), iliyoanzishwa kisheria mwaka 1986, nayo inanyoosha mikono imebeba haki ya jukumu kuu la kuwa Mshauri Mkuu wake katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU) nchini.

Ndani yake inasema, sasa inatumia huduma zake kiuchumi kunufaisha nchi katika mahitaji yanayoangukia mahitaji yao kiuchumi.

Hadi sasa, inawajibika kisayansi kwa maendeleo ya teknolojia nchini kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia (MTUSATE), ikitoa ruzuku kugharamia utafiti, teknolojia na ubunifu nchini.

Chanzo kikuu cha fedha za mfuko serikalini zinatumika kujenga, kukarabati na kununua miundombinu na vifaa vya maabara, katika taasisi za utafiti na maendeleo, ili kuwapatia ruzuku wabunifu wa maeneo mbalimbali nchini.

Hapo inajumuisha kugharamia miradi ya utafiti, uwezeshaji, uhalalishaji teknolojia na kusambaza matokeo ya utafiti na ubunifu, pia ajira.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, anaiambia Nipashe kuna mafanikio katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2023, serikali kuongeza pato la serikali kupitia MTUSATE, kutoka Sh. bilioni 3.5 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 4.4 mwaka 2021/22.

Dk. Nungu anataja mafanikio mengine, ni miongozo sita ya kuendeleza utafiti na ubunifu nchini, inayoandaliwa na kuanza kutekelezwa, pia kwa wadau maendeleo.

Anasema fedha za MTUSATE zimeongezeka, ikilinganishwa na mwaka 2021, kutumikia katika mambo mbalimbali.

Pia, anataja matumizi ya kuchangia uendeshaji Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) nchi nzima na kuendeleza wabunifu uliopatikana kupitia mafunzo ya ubunifu, ushauri, kuwaunganisha na taasisi kisekta, kulingana na mahitaji yao ya ruzuku.

Hapo anatoa mfano, mshiriki wa MAKISATU 2020 mwenye ubunifu wa Mita za Kulipia maji kabla ya matumizi amewezeshwa kuunda kampuni changa.

Anasema kampuni tanzu chini ya COSTECH, imeingia makubaliano na Mamlaka ya Maji Vijijini (RUWASA) mwaka 2021/22 kuwa mteja mkuu, ikipewa fursa kufunga mita hizo mikoa yote 25 ya Tanzania Bara. Hadi sasa imeshafunga mita 20 katika mikoa; Tanga, Pwani, Morogoro, Iringa na Njombe.

Dk. Nungu anafafanua, ni fedha zimefadhili miradi 10 ya utafiti kwa Sh. 2,281,119,320; mitatu ya miundombinu ya utafiti, ikiwamo katika maeneo ya afya (tiba asili), mifugo na uvuvi katika Taasisi ya Chanjo Kibaha (TVI - Kibaha), Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na Taasisi ya Tiba Asilia (ITM) iliyopo katika Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili, yenye jumla ya gharama ya 1,188,397,320/-

Pia, kuna miradi mitatu ya kitafiti katika maeneo ya kilimo na Uvuvi kwa taasisi ya TARI-Mikocheni, UDSM na SUA iliyogharimu kiasi cha Sh. 360,000,000.

Pia, kunatajwa miradi minne ya utafiti katika maeneo ya kilimo na viwanda kwa taasisi za vyuo vikuu kadhaa, zikigharimu Sh. 732,722,000.



Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

**UTAFITI WABORESHWA**

Dk. Nungu anasema, COSTECH imeratibu na kuzindua miongozo sita ya utafiti, katika kusudi la kuendeleza ubora wa viwango vya utafiti nchini.

Inadhamiriwa kwa miaka mitano ijayo, 2021/22 hadi 2025/26, tume inawezesha taasisi nane zenye mamlaka za kusimamia tafiti kisekta, nne Bara na nne visiwani.

**WASHIRIKA WA MAENDELEO**

D. Nungu anaitaja COSTECH ni mwanachama wa asasi Global Research Council (GRC), ambayo ni sehemu ya mataifa 11 kutoka mabara manne; Afrika, Ulaya, Asia na Amerika Kusini duniani.

"Mchakato wa kuwapata washindi unaendelea na kuongeza watafiti sasa wamekaribishwa kwa hatua ya kuandaa maandiko yao," anasema Dk. Nungu.

Anafafanua, nia ni kujengwa uwezo na ujuzi kwa watafiti, kujenga mtandao, pia kuongeza maarifa kwa watafiti, ili kuwezesha kuwapo tafiti zenye tija kwa matokeo chanya kwa jamii.

Anaeleza, COSTECH imeshafahamika kimataifa kwa tija na inaomba kuwa mdau katika kundi la wataalamu wanaojadili usawa katika ubia wa ngazi ya wafadhili.

Lingine linatajwa ni COSTECH kushiriki katika mradi wa kukuza ubunifu kusini mwa Afrika, ambayo ni ushirikiano kati ya serikali ya Finland na nchi tano za Afrika; Tanzania, Msumbiji, Namibia, Botswana na Afrika Kusini.

Hapo Tanzania ilishafanikiwa kupata Sh. bilioni 2.030 (Euros 720,000) kwa miradi mitano iliyotekelezwa nchini.

Pia inatajwa kuna Sh. milioni 100 kwa Watanzania walioshiriki miradi ya SADC, ikijivunia ni kwamba kupitia mradi wa KItanzania, kumepelekwa ubunifu wa ubinfu kwa taasisi kama; Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, nchini Zambia.

Hapo kwa miradi ya ubunifu, COSTECH imekuwa sehemu ya timu iliyopata miradi miwili kutoka Umoja wa Ulaya kupitia Atamizi yake (DTBI) na Ukumbi Bunifu (BUNI):

COSTECH kupitia kampuni tanzu DTBI, inashiriki katika mradi uitwao Hubiquitous, unaolenga kuanzisha na kukuza ushirikiano baina ya bara la

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

# HIFADHI KITULO NA UPEKEE WAKE;

## • Vivutio maua, ndege wanaosafiri kutoka Ulaya • Ukingoni mwa milima alikopita Dk. Livingstone

**Na Mwandishi Wetu**

NI kilomita 110 kutoka jijini Mbeya kuelekea Kusini Mashariki inakopatikana Hifadhi ya Taifa Kitulo, maarufu Bustani ya Mungu.

Mahali hapo panaunganisha vilele vya milima Kipengere, Uporoto na safu za milima ya Livingstone alikopita Dk. David Livingstone, ikiundwa na mipaka ya wilaya za Makete (Njombe), Rungwe na Mbeya Vijijini (Mbeya).

Kijiografia, pana baridi sana ikielezwa miezi Desemba na Aprili, pia Juni hadi Agosti, hufikia nyuzi joto sifuri na katika hali ya kawaida, huwa nyuzi joto saba. Utajiri wa mvua nao upo, Oktoba hadi Mei, ni wastani wa milimita 1,500 hadi 1,700.

Ukubwa wake ni kilomita za mraba 412.9 ndani ya mwinuko kati ya mita 2,100 hadi 3,000, ikiwa ni hifadhi ya kwanza barani Afrika mahsusi kwa ajili ya kutunza mimea, hasa jamii ya maua.

Mkuu wa Hifadhi Kitulo, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Theodora Batiho, anatoa historia, awali palijulikana Elton Plateau, baada ya kugunduliwa na mtafiti Fredrick Elton, aliyepita hapo mwaka 1870.

Anasema, mwaka 1960 Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), lilichukua eneo hilo kulimia ngano na kufuga kondoo. Baadaye, paligeuzwa shamba la ng'ombe ambalo, mradi unadumu hadi sasa.

### KULIVYOTANGAZWA HIFADHI

Mkuu huyo anasema, hatua za kupafanya Hifadhi ya Taifa zilianza mwaka 2002 na kufanikishwa 2005, akimtaja mhifadhi wake wa kwanza, William Mwakilema, ambaye sasa ni Mhifadhi Mkuu wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Ziara ya mwandishi hivi karibuni, alishuhudia uzuri wa hifadhi yenye aina 45 za maua, huku baadhi yake yanapatikana hifadhini Kitulo peke yake duniani, yakiwa na tabia ya kuchanua kila mwezi Novemba hadi Aprili kila mwaka.



### NDEGE WAHAMIAJI

Theodora anasema kuna ndege aina ya Great White Stork (abdmin stork) wenye uwezo wa kuruka kutoka eneo la Ulaya Mashariki na wengine kutoka Afrika Kusini, wakisafiri umbali kilomita 7,000 kwa siku 322. Wana kawaida ya kutaga na kuangua mayai mengi, kabla ya kuanza safari ndefu.

Ofisa Uhifadhi Daraja la Kwanza - Utalii, Susan Tesha, anafafanua sababu ni mazingira yake salama na rafiki kwao kuzaliana, huku chakula ni kingi, pia hifadhini Kitulo, kunapatikana ndege wengine kama vile Blue Swallow wanaotumia hifadhi kama makazi yao ya misimu.

Anataja kuwapo aina za nyani Kipunji, waliogunduliwa mwaka 2003, pundamilia walioletwa kutoka Hifadhi ya Taifa Mikumi na swala kutoka Ruaha.

Hao anawataja kuendana na vipepeo wanaosaidia kuchavusha maua, vinyonga, mijusi na vyura, wote wakiongeza utajiri wa kibailojia hifadhini Kitulo, wakiishi kwenye uwanda tambarare, mabonde,vilima na maporomoko ya maji na mabwawa, yanachangia maji yake kwenye Mto Ruaha Mkuu, tegemeo kwa Hifadhi ya Taifa Ruaha, mabwawa ya kuzalisha umeme ya Mtera mkoani Dodoma na Kidatu, Morogoro.

Susan anasema, ni ukanda wa mvuto, upepo mzuri unapopambwa na sauti za ndege unaofariji masikio yao, akiwa katika mahali anapashudia vizuri bondeni, Mlima ya Rungwe, Ziwa Nyasa na milima Livingstone, pia maporomoko yanayozalisha maji Mwakilema na Mwakipembo.

### KUNAVYOFIKIKA

Anasema, Kitulo kunafikika kirahisi mtu akitokea Mbeya Mjini umbali wa kilomita 110, vilevile umbali wa kilomita 70 kutoka Igawa wilaya ya Mbarali au mjini Makete, huku akishauri muda mzuri kuzuru mandhari ya maua yanayochanua, ni kuanzia Desemba hadi Aprili, huku utalii wa kupanda milima ni kuanzia Juni hadi Agosti, penye baridi kali.

Mwandishi wa makala, aliyekutana na mtalii kutoka Hispania, Marc Antillachraia, anaeleza kilichomvutia Kitulo ni mimea, maua, viumbe na maporomoko ya maji, ikiwa sehemu ya maeneo alikonuia kuzuru barani Afrika, akiahidi kuwa balozi mzuri wa hifadhi hiyo, atakaporudi kwao.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mafiga, kijiji jirani cha Missiwa, wilayani Makete, Laynada Mwasanga, anasema hivi karibuni walipeleka wanafunzi hifadhini Kitulo, kuona uzuri wa maua, mimea na wanyama.



Aina ya maua na mandhari, kivutio cha watalii kuyafuata Kitulo, kutoka safari ya mbali ughaibuni. Picha ndogo kulia; ndege adimu duniani White Stork, wanaopatikana hifadhini Kitulo. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

Shule iko jirani, ila wanafunzi walikuwa hawajawahi kutembelea.

Ni hatua kama hiyo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Kinyika wilayani Makete, Faida Ngulo, naye karibuni alipeleka wanafunzi hifadhini kujifunza na kuburudika na vilivyomo.

### MATATIZO YAKE

Kamishna Theodora anasema, hadi sasa wanakabiliwa na shida kadhaa, ikijumuisha kiwapo miundombinu duni ya vumbi kufika hifadhini Kitulo na wakati wa mvua hali inakuwa ngumu zaidi.

Vilevile kuna utata wa wakulima kuvamia maeneo ya Hifadhi Kitulo akinyoosha wengine kuingia kuchimba viazi mahali hapo. Hapo anasema "tunaomba barabara hizi ziboreshwe kwa kuwekewa lami zitatusaidia kuongeza idadi ya watalii."

Anadokeza kwamba, serikali iko katika hatua ya kujenga barabara kiwango cha lami kutoka Makete Mjini, kupita hifadhini Kitulo hadi Mbeya, akisema itawafungulia watalii wengi zaidi.

Lingine analitaja ni mwitikio mdogo wa wawekezaji wa hoteli ndani na kando ya hifadhi, kuwezesha watalii kupata pa malazi.

Naibu Kamishna wa Uhifadhi Kanda ya Kusini, Steria Ndaga, anakiri kufahamu tatizo hilo, pia ujenzi wa barabara ya lami, Makete hadi Mbeya.

Anataja matatizo mengine ya hifadhi kanda yake; Ruaha, Katavi ambako kunaongoza kwa uvamizi, kuliko Kitulo. Ndaga anasema wamekuwa wakiyakabili kwa hatua za kisheria zilizoko, hata imesaidia kupunguza uvamizi huo.

### MIKAKATI WAENDAKO

Kamishna Msaidizi Theodora, anataja kuna mikakati ya miaka mitano kukuza utalii hifadhini ni Kitulo, ni kujenga nyumba za kulala wageni na kuitangaza Hifadhi ya Kitulo kupitia maonyesho.

Mingine ni kuelimisha wanafunzi shule za msingi na sekondari jirani kuhusu uhifadhi, ikiwa njia ya kuwapandikizia uzalendo wanaoishi kando ya hifadhi. Hadi sasa tayari baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi Mafiga na Matamba, pia sekondari za Matamba na Kinyika, wilayani Makete wameshatembea hifadhi kuona vivutio.

Anasema, wanaendelea kuhamasisha wanaoishi kando ya hifadhi kutembelea na hadi sasa kuna mafanikio, kundi la wanawake 40 walizuru Desemba 2022 mwaka jana.

Mkakati mwingine ni kuanzishwa utaratibu, wageni kubebwa na punda na farasi hifadhini, utalii wa kutumia baiskeli, pia kuanzishwa mashindano ya mbio za masafa marefu yaani 'Kitulo Marathon'.

Vilevile anataja matarajio ya utalii wa maombi, waumini wa madhehebu mbalimbali wakifika na kufanya maombi katika maeneo tulivu ya hifadhi, ikiwamo milima midogo na mikubwa iliyopo.

Maharusi nao sasa kupewa fursa kutembelea hifadhi hiyo, kwa ajili ya kupiga picha na kumpumzika wakati wa 'fungate' wakitangaza vivutio kwa kutumia mabango.

# Safari ya mvuto, mjasiriamali wa urembo kutoka binti hadi amekomaa kiumri

**Na Christina Mwakangale**

UREMBO ni miongoni mwa shughuli zinazokua zaidi nchini. Pendo Shuma, ni miongoni mwa wadau. Fuatilia anavyoielezea Nipashe.

**Swali: Kwa kujitambulisha, unaielezeaje historia yako?**

**Jibu:** Naitwa Pendo Lameck Shuma, mwanzilishi na mmiliki wa Lavie Cosmetics nilianza kazi kama miaka 13 iliyopita na tulianza kwa huduma za make up mbalimbali na ilikuwa ni huduma ya mobile (huduma tembezi) yaani unapiga simu nakufuata na nilikuwa nimeajiriwa kipindi hicho na nilikuwa naiba muda walau kidogo, ili nifanye biashara.

Baadaye nikaamua kuhamia kwenye biashara kabisa nikaomba likizo bila malipo ya miezi mitatu na nikaona milango inafunguka na nikatafuta vyumba viwili maeneo ya mikocheni nikapata na kufungua ofisi rasmi tulikuwa tumepanga watu wawili baada ya mwaka nikatafuta nyumba ambayo tulikuwa tunachangia na mwenzangu, Kijitonyama.

Kwa sababu biashara ilikuwa inakuwa kubwa, ikanibidi nitafute nyumba kubwa tena nikarudi Mikocheni na huko nilikaa kama miaka mitatu, minne kwenye vyumba viwili ikanipasa sasa nitafute nyumba kubwa. Na hii nyumba sasa ni miaka minne.

**Swali: Unapata wapi malighafi kwa ajili ya kuhudumia wateja wako?**

**Jibu:** Biashara inavyokua nikagundua fursa nyingine ambayo ni vitendea kazi. Ilikuwa inatuwia vigumu kidogo kwenye vipodozi na ukitaka vitu vizuri inabidi uagize kutoka nje. Ikabidi tuanze kutengeneza vipodozi vyetu na hapo ikazaliwa Lavie Cosmetics.

Kuna vifaa vya aina zote kwa wanaotaka kujifunza zaidi vifaa vipo vya kila aina na duka la vipodozi lipo Mikocheni na Kariakoo na hapo hapo tukafungua shule ya kuwafundisha mambo ya urembo watu wengine wanaopenda.

**Swali: Hadi sasa mmefundisha watu wangapi, Je, wengi wao ni wanawake au pia wanaume?**

**Jibu:** Tumefundisha watu wengi na tumeanza kufundisha mwaka 2016 na wanafunzi ni zaidi ya 40 na wengine walikuwa ni wafanyakazi wetu wakaweza kujiajiri na wanaokuja kujifunza mara nyingi ni wanawake.

**Swali: Ni wapi unapata malighafi kwa ajii ya kutegeneza bidhaa za vipodozi?**

**Jibu:** Malighafi tunaagiza China, Uturuki, Thailand. Mzigo unafika baada ya wiki nne, zamani ilikuwa ni usafirishaji ni wa ndege na gharama kubwa ila sasa kwa meli ni nafuu zaidi.

**Swali: Wapi ulipata mafunzo haya na je, kwa nini urembo si shughuli nyingine?**

**Jibu:** Nilijifunza kupitia You tube (mtandaoni) wakati nafanya kazi kampuni ya ndege nilikuwa 'air hostess' na kuna wakati unafanya kazi kwa kuwa juu juu, unakuta labda mwenzio anaumwa, inabidi wewe uingie kwa niaba yake unakaa ofisini saa saba na saa hizo nikiwa kazini naangalia 'you tube' na ndio nilipojifunzia huko zaidi.

Nilikuwa napenda sana mambo ya urembo kwa sababu hata nyumbani nilikuwa nafanya hivyo. Ilitokea tu kwamba nyumbani pakiwa na shughuli yeyote mimi nitawapamba.

**Swali: Je, baada ya hapo ulijiendeleza, yaani kuwa mwanataaluma rasmi kati urembo?**

**Jibu:** Nilijiendeleza wakati tayari nimeshafungua biashara, kwa sababu sehemu zingine unaenda wanahitaji vyeti, lazima uwe navyo, ili niweze kufundisha wengine. Kozi nilifanyia Dubai (Falme za Kiarabu), mwaka 2016. Mabadiliko ni makubwa na vitu vinatoka kila wakati na hata baada ya kumaliza mafunzo niliendelea kujifunza pia mtandaoni.

**Swali: Kwa nini urembo ni ghali na hili linasemwa sana na wateja?**

**Jibu:** Hata gharama za mafunzo ni kubwa, kwa sababu 'make up' sio bei rahisi kama wanavyofikiria, ni gharama mno kweli! Mimi nilipokwenda kujifunza, pia nililipa kiasi cha shilingi milioni 5.6 na hapo bado hujalipia malazi, chakula, usafiri.

Na mafunzo yalikuwa siku 14, hivyo inakuwa gharama kujifunza kwa sababu vifaa pia ni ghali mno na tunajitahidi kupunguza, lakini bado bei inakuwa vilevile haipungui.

**Swali: Ulikuwa na wito wa kufanya biashara hiyo?**

**Jibu:** Nilikuwa napenda, kufanya biashara tangu nikiwa bado mdogo na wakati niko chuo nilikuwa nafanya biashara na wakati nimeajiriwa nilikuwa sipati kile ninachotaka. Nimeajiri vijana wengi, ingawa wakati wa Uviko-19 biashara iliyumba, lakini sasa tunapambana.

**Swali: Je, unakabiliana na changamoto gani?**

**Jibu:** Changamoto kubwa ni kuwa wateja wakija hapa huwa wananitaka mimi niwahudumie, bila kujua wapo wanaoweza vizuri, nimewafundisha mwenyewe na pia akitaka nimfanyie mimi bei inakuwa tofauti kidogo.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wasanii hamasisheni kilimo na si matusi na 'kiki' zenu






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

NAPENDA sana muziki, kuupiga, kuusikiliza na kuucheza. Wapo watu wanasema muziki ni dawa na ni kwa sababu, huburudisha na huelimisha pia jamii.

Mwanamuziki wa Kikongo, Ramadhani Ongala, ambaye sasa ni marehemu, aliimba wimbo ukisema muziki ni wito, muziki ni fundisho, muziki ni maombolezo na kwamba hata kwenye matukio ya kiserikali, muziki ndio hukusanya watu.

Tumeshuhudia katika matukio mbalimbali, ambao kweli muziki ndio hukusanya watu na kuwaweka pamoja na kuimba kwa ama kuwasherehesha au kuwafariji, hasa wanapokuwa kwenye simanzi.

Ongala, maarufu kama Dk. Remmy katika ghani zake, akasema mbele ya (kabla ya) Mwenyekiti kuhutubia, muziki ndio huwakusanya watu. Na katika muziki huo, ndipo elimu au ujumbe fulani hutolewa kwa jamii.

Zamani, muziki ulitokana na zana duni kama pembe za wanyama, ngoma na nyingine zilizotoa milio na kufurahisha watu kwa kusikiliza na hata kucheza. Leo hii, kuna vifaa vya kisasa vitumiavyo umeme.

Lakini, zamani pia watu walitunga nyimbo zilizobeba ujumbe mzito wenye elimu kwa jamii. Watu hao wakiimba mmoja mmoja au hata katika makundi na kwa kweli ilifana.

Hakuna sherehe tangu zamani, ambazo zilipita bila kuhusisha muziki, uwe utumiaji zana au bila zana, kwa maana ya nyimbo tu, ili mradi haukuachwa bila kuhusishwa kwenye sherehe na hata misiba.

Muziki umeendelea kutumika hadi leo, makanisani watu wanaimba, misikitini watu wanaimba, shuleni, vyuoni na maeneo mengine yanayoruhusu mikusanyiko ya watu.

Katika mikutano ya hadhara hususan ya kisiasa, muziki ni kitu kinachotumiwa sana kuvuta umati wa watu hata wasio wafuasi wa chama husika, kwa sababu wapo wanaoenda kumuona msanii, mwanamuziki au tu kusikiliza muziki wenyewe.

Tanzania kwa miaka mingi, imekuwa na wanamuziki wa muziki wa dansi na wa taarabu, pia ikawa na vikundi vya nyimbo na ngoma. Wote hawa wamekuwa wakitumika katika kumbi za kidini na zisizo za kidini.

Tanzania imekuwa na wasanii, baadhi yao wakijiita wa kizazi kipya yaani Bongofleva, nao wakija kwa mahadhi yao tofauti tofauti na zilivyo bendi za muziki wa dansi. Na hawa hupendwa sana na vijana.

Wanamuziki wa dansi kihistoria walikuwa wakitumiwa katika shughuli mbalimbali, hususani za kiserikali, si katika kutumbuiza tu, lakini hata katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu jambo fulani.

Tunakumbuka operesheni mbalimbali zilizoendeshwa na serikali kuhusu masuala ya afya, kilimo, makazi, michezo na elimu. Bendi zilitunga nyimbo na kuelimisha watu kuhusu lishe bora, kilimo cha kisasa, nyumba bora na elimu bora kwa Mtanzania ikiwamo elimu ya watu wazima.

Bendi zote lilipotokea jambo, zilitunga nyimbo na kuzirekodi haraka hata zikasikika redioni, wananchi wakasikia na kuhamasika kufanya jambo kusudiwa. Hata katika vita vya Kagera, kuna bendi zilitunga nyimbo za kuhamasisha wapiganaji na wananchi.

Nyimbo zote hizo zilikuwa na maneno yenye staha, walioziimba walifanya hivyo kwa staha pia, wakijua umuhimu wao na kile walichokifanya kwa jamii iliyowatazama na kuwasikiliza.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan kupitia kwa msanii wa mashairi, Mrisho Mpoto 'Mjomba', alitoa mwito kwa wasanii kwenda kutoa elimu na kuhamasisha kilimo kwa wananchi, hususan wakati huu ambao Taifa linawekeza katika kilimo zaidi.

Alichokifanya Rais, akimtaka Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe aratibu mpango huo, ni kizuri na chenye nia njema ya kuhakikisha elimu hiyo kuhusu kilimo kupitia mpango wa BBT, kinafikia watu kikamilifu.

Wasiwasi wangu ni kwa baadhi ya vijana hawa wanaotakiwa kulifanya hilo, wanaongoza kwa kuimba nyimbo zenye mahadhi ya Afrika Kusini na Nigeria, lakini zenye maneno taka yasiyostahili kusikilizwa, si tu na wakulima, lakini na Watanzania wote wanaojitambua.

Hivi kwa muziki wao huo na kwa lugha yao hiyo, ujumbe utafika sawasawa kwa Watanzania wanaojua nini maana ya kilimo na upi umuhimu wa kilimo kwao?

Tuombe Mungu wakajisahihishe na kuimba nyimbo nzuri zisizo na ujumbe ufike kunakokusudiwa, bila ya kusababisha taharuki. Ni dhahiri, msanii wa Tanzania anapopata fursa kama hiyo hutaka kama si kutafuta kiki, basi aonekane sawa na mwanamuziki wa Afrika Kusini au Nigeria, basi hatachelewa kuimba matusi. Hatutakubali. Alamsiki!

UCHUMI

# Serikali, wadau binafsi wakutana ‘kukuna vichwa’ kisa halmashauri hazikopesheki

**Na Neema Emmanuel,**

**MWANZA**

MIONGONI mwa matatizo yanayokabili mamlaka za serikali za mitaa nchini, ni kwa halmashauri nyingi kukosa uwezo wa kuandaa maandiko ya miradi yanayokidhi vigezo vya kupata fedha au kukopesheka, hata ikatekeleza mipango yake ya maendeleo.

Hilo limeifanya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango, kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), kuandaa kongamano la utekelezaji mpango mikakati kwa halmashauri nchini.

Ni majadiliano ya siku mbili jijini hapa, kati ya tarehe 9 na 10 mwezi huu, ukihusisha Halmashauri za Jiji la Mwanza, Tanga na Halmashauri ya Manispaa Ilemela.



Sehemu ya Jiji la Mwanza, iliyokuwa mwenyeji wa mjadala. **PICHA: MTANDAO**

Akiwasilisha mada, Meneja Uendelezaji Biashara na Uwekezaji wa Benki ya Maendeleo ya Tanzania (TIB), Joseph Chilambo, anasema halmashauri nyingi zinashindwa kuandaa miradi hata zikakopesheka.

Chilambo anafafanua hata inapotokea zinakopesheka, hubaki na tatizo la kukosa uwezo wa kurejesha fedha kwa wakati, akitoa mfano benki hiyo hadi sasa, imetoa mkopo wa shilingi bilioni nane, lakini zilizorudishwa ni shilingi bilioni 1.8 pekee.

Anataja shida ni uwezo mdogo wa kurejesha mikopo ya kibiashara, kifedha, kijamii na kimazingira, huku zikikosa usimamizi madhubuti wa utekelezaji miradi husika.

“Uratibu sahihi wa mipango na wadau mbalimbali kwenye miradi yenye manufaa ya kibiashara, inapaswa kufadhiliwa kupitia vyanzo vya kibiashara kama mikopo ya benki, ushirikishwaji wa sekta binafsi, matumizi ya hati fungani za kimataifa au dhamana na vifaa kwa ajili ya utoaji wa huduma za umma zinazotarajiwa,” anasema Chilambo.

Kaimu Ofisa Muidhinishaji wa Mfuko wa EDF katika Wizara ya Fedha na Mpango, Jonathan Mpuya, anakiri watendaji wengi wa halmashauri, uwezo wao ni mdogo kuandaa maandiko ya mradi na ni moja ya eneo linalopaswa kufanyiwa kazi katika mradi anaouita ‘Green and Smart Cities’ au ‘Sasa” Project.’

Anaeleza, hata mjadala husika unagusa mifano ya miradi ambayo haijafanyiwa upembuzi yakinifu na uwezo mdogo wa halmashauri kuikabili.

Hapo, Mpuya anaitolea fafanuzi kwamba, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, imeamua kufanyia kazi, kwa kuongezea uwezo halmashauri nchini, zipate fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati, kama ilivyopangwa.

“Dhumuni la majadiliano hayo ni moja ya kiashiria tulichokubaliana na Umoja wa Ulaya kwamba halmashauri husika zitekeleze miradi ya maendeleo na kuwa na miradi yao ambayo itazungumzia mipango mikakati yao,” anaeleza.

Anadokeza angalizo lao la awali, serikali imewashirikisha wadau wa taasisi za fedha, sekta binafsi, taasisi za elimu ya juu na asasi zisizo za kiserikali, kwani baadhi ya miradi siyo lazima itekelezwe na halmashauri.

“Miradi hiyo inatakiwa kuwa inafadhiliwa na fedha za halmashauri yenyewe, lakini na vyanzo vingine vya mapato ambavyo vinaweza kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa. Pia, taasisi za kifedha zione kuwa zinaweza kuingia katika kuunga mkono miradi na waone kuna fursa,” anaeleza Mpuya.

**HATUA ZA KISERIKALI**

Mratibu wa Programu ya Uimarishwaji Mikoa na Serikali za Mitaa (RLGSP) kutoka TAMISEMI, Lemmy Shumbusho, anasema wamegundua halmashauri nyingi zinashindwa kuandaa mpango mkakati unaotekelezeka.

Hapo anataja, jitihada za kuwapa mafunzo watendaji wa halmashauri na kuwaandalia muongozo wa utekelezaji miradi.

Pia anafafanua kuwa halmashauri zimekosa fedha za kutosha kutekeleza miradi, hivyo wanawatafuta wadau kuhamasisha miradi ya ushirikiano, wakizihimiza halmashauri kuwekeza katika miradi ‘inayolipa’ ili zijisimamie.

**MWANAZUONI ANENA**

Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, Dk. Titus Mwageni, anashauri uhamasishaji taasisi za fedha za mtaji ni muhimu, kwani bajeti za mamlaka za serikali za mitaa ni ndogo kukidhi wawekezaji.

Anafafanua halmashauri za jiji, manispaa na wilaya ni taasisi muhimu katika kuleta maendeleo ya wananchi wote nchini.

Dk. Mwageni anataja ulingo wa tatizo ni kwa halmashauri kushindwa kutekeleza mipango waliojipangia, ikiwamo kukosa fedha, pia utaalamu wa kusimamia, maandalizi na tathmini ya miradi inayokosa matokeo chanya.

“Halmashauri nyingi haziwezi kuwa na fedha za kutosha kuwekeza katika maeneo muhimu ya uwekezaji na hivyo sekta binafsi zinaweza kuwa suluhisho zuri katika uwekezaji unaopendekezwa,” anaeleza.

Anasema matatizo ya ubia kati ya halmashauri na sekta binafsi yako katika sera na kisheria, zinapobeba urasimu, hata kuwakatisha tamaa wawekezaji binafsi wanaonuia kuunga mkono juhudi hizo serikalini.

“Kuunda mwongozo wa msingi wa takwimu na taarifa za uwekezaji wa kikanda au wilaya baada ya LGAS kupanga na kuteua maeneo ya uwezekano wa uwekezaji kunapaswa kuwa na kanzi-data ya miongozo, ambayo taarifa zote za uwekezaji kwa halmashauri fulani zitakusanywa na kupatikana kwa wawekezaji na wadau wengine kutoka ndani au nje ya mamlaka,” anaeleza Dk. Mwageni.

Dk. Mwageni anataja umalizaji tatizo upo katika halmashauri kuwajengea uwezo kitaalamu, watumishi wake kuandaa mipango, kuitumia, kuifanyia tathmini, hata usimamizi wa mipango kwa ujumla.

“Suluhisho ni halmashauri kuja na miradi ya kimkakati ya kuweza kupata fedha, ili ziweze kupata fedha na kusimamia utekelezaji wa mipango hii...”anaeleza, akitaja kinyume chake ni kutofanikiwa.

Anaendelea: “Halmashauri ikishirikiana na sekta binafsi kuanzisha miradi mbalimbali ya kibiashara, sekta binafsi itapata faida na italipa kodi kwenye halmashauri zetu na ikatumika kutoa huduma mbalimbali.”

**TAMISEMI/ WADAU**

Mkurugenzi Msaidizi wa Maendeleo ya Miji na Vijijini kutoka TAMISEMI, Rachel Kaduma, anasema wameboresha mifumo ya kukusanya mapato na sasa upo wa kielektroniki unaoitwa ‘Tausi’.

Pia Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Myfish Tanzania, Elipidius Mpanju, anataja nafasi ya sekta binafsi ni kutengeneza mpango mkakati unaohusika moja kwa moja kutunga sera nchini.

“Serikali haiwezi kufanya vitu vyote, vingine vinaweza kufanywa na sekta binafsi na kuwapunguzia gharama na muda na ikafanyika kirahisi.

“Mathalani, leo hii nikitaka kumtafuta mtaalamu anaweza kwenda nchi nyingine nikamchukua mtaalamu na kufanya naye kazi, lakini serikalini lazima ufuate utaratibu unaochukua muda mrefu,” anadems Mpanju.

Meneja Programu ya Maendeleo ya Miji Umoja wa Ulaya Tanzania, Martino Vinci, anaahidi Umoja wa Ulaya utaendelea kufadhili mradi huo na kuzitaka halmashauri zitumie kwa kushirikiana na sekta binafsi.

## Bosi COSTECH: Miaka miwili kiserikali, tunaneemeka kwa teknolojia uchumi

**INATOKA UK.11**

Afrika na Ulaya, kwenye ubunifu wa kidigitali unaoshirikisha kampuni changa za teknolojia ya digitali, kutoka nchi tano za Afrika na nne Ulaya.

Barani Afrika, nchi zinazoshiriki ni Tanzania, Kenya, Ghana, Misri na Nigeria, kila moja ikiratibu ushiriki wa kumbi bunifu tano kwenye nchi husika.

Dk. Nungu anasema Tanzania imeratibu upatikanaji na ushiriki kwenye mradi 10, ikwamo kupitia taasisi; SIDO Tech hub (Arusha), SUZA Tech Hub (Zanzibar) , Bonge Tech (Dar es Salaam), Capita space (Dodoma) na Buni Hub (Dar es Salaam), akinena ni jambo la kujivunia.

Hadi sasa Tanzania imeshaandaa kitabu kinachoelezea mfumo wa ubunifu barani Afrika, ili kuimarisha uhusiano wa kampuni changa zilipo Afrika na Ulaya, kwenye teknolojia ya kidigitali.

Dk. Nungu anafafanua, COSTECH kupitia ukumbi wake wa ubunifu (BUNI Hub) inashiriki katika mradi wa AfriconEu, lengo ni kuunganisha kumbi za ubunifu kutoka bara la Afrika na za bara la Ulaya.

Anasema jumla ya kumbi za ubunifu 11 zinashiriki kutoka Afrika; Tanzania, Uganda, Ghana na Nigeria na nchi za Ulaya ni; Uingereza, Ugiriki Italia, Ureno na Slovenia.

Pia, anasema, wanaendelea na mazungumzo na Shirika la Maendeleo la Sweden (Sida), lifadhili utafiti kwa miaka mitano, wakiwa wametenga Sh. bilioni 10.

Inaelezwa pia, COSTECH inanufaika na uwekezaji uliofanywa na serikali ya awamu iliyopo, kupitia mradi wa Mageuzi ya Elimu na Uchumi wa Juu, wastani wa Sh. bilioni 18.4





# Maendeleo ya Jamii yapongezwa hatua upitiaji mitaala

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

IDARA ya Maendeleo ya Jamii imepongezwa kwa kuanza mchakato wa mapitio ya mitaala ya programu za maendeleo ya jamii na uhandisi ujenzi kwa wakati.

Pongezi hizo zilitolewa jana jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. John Jingu, alipokuwa akifungua warsha ya mapitio ya mitaala ya uhandisi ujenzi na maendeleo ya jamii.

Dk. Jingu alisema hatua hiyo itasaidia vijana wanaojiunga na vyuo pamoja na vyuo vyote vitakavyotumia mitaala hiyo wapate mafunzo yanayoendana na mazingira ya sasa.

"Niwashukuru NACTVET kwa jinsi ambavyo mmekuwa mstari wa mbele katika kutoa miongozo mbalimbali ya kuboresha mafunzo. Vilevile ninawashukuru washiriki wote mliofika hapa kwa ajili ya kutoa maoni kwenye mitaala hii,"alisema.

Aidha, Dk. Jingu aliwataka kuhakikisha mitaala watakayotumia kutoa mafunzo inaakisi hali halisi ya mazingira ya jamii na mahitaji ya nchi na dunia kiujumla.

"Mitaala ni lazima izingatie jamii imebadilika kiasi gani kufuatia mabadiliko ya kiteknolojia, kisiasa na kiuchumi yanatokea duniani na hata nchini kwetu," alisema Dk. Jingu.

Alieleza kuwa kada ya maendeleo ya jamii inatazamiwa kuwa itachangia katika kuisukuma jamii mbele iwapo itazingatia uhalisia.

Hata hivyo aliwaagiza kuwa na mahusiano ya karibu baina ya wadau wa mitaala na vyuo hasa katika maeneo yao ili kuwezesha taasisi hizo kuvuna wanafunzi ambao wana picha ya hali halisi ilivyo katika jamii.

Alisema: "Nyie mkienda kule mnawasaidia kuwapa picha ya hali halisi ilivyo inawezekana mkiachia walimu waliopo pale wanawapa kwa nadharia ili baada ya hapo tutoke na mtu aliyekamilika anauzoefu kupitia maarifa ambayo tunawapa lakini vilevile ana nadharia ambazo zinahitajika," alisema.

Mkurugenzi Msaidizi wa sehemu ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Neema Ndoboka, alisema mitaala ambayo inapitiwa ni maendeleo ya jamii na ufundi kwa ngazi ya cheti ambayo iliandaliwa tangu mwaka 2018.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Happy Hiza, alisema kuwa ni wakati sasa mitaala kujumuisha taaluma za kuwashawishi wananchi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya serikali.

# TEMESA yashauriwa kujiendesha kibiashara

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, ameutaka Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) mkoani humo kujiendesha kibiashara ili kuipunguzia mzigo serikali kutokana na kutoa fedha nyingi kuendesha taasisi hiyo.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua kikao cha wadau na karakana ya Mkoa wa Singida ambacho pia kilihudhuriwa na Mkurugenzi wa Matengenezo na Huduma za Ufundi TEMESA Dodoma, Mhandisi Hassan Koronda.

"Tengenezeni magari kwa ubora na weledi punguzeni gharama za uendeshaji ili muisaidie serikali na mkimbiliwe na wateja," alisema.

Aidha, Mganga aliwataka TEMESA kutumia fursa waliyonayo kutoka nje kujitangaza ili wafahamike badala ya kukaa tu ofisini na akaishauri kuanza kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya kupata mrejesho kutoka kwa wateja wao kupitia ujumbe mfupi.

Mganga alihimiza TEMESA kutoa mafunzo kwa madereva ya uendeshaji wa magari ili wajue mbinu ya kuyatunza ukizingatia kuwa ni wadau wao na akaomba waanzishe kitengo cha uoshaji wa magari ili iwe motisha kwa wateja wanaowapelekea vyombo vyao vya moto.

Akizungumzia madeni yanayodaiwa na TEMESA aliomba apewe orodha ya wadaiwa wote zikiwapo taasisi za serikali ili aweze kuonana na wahusika waanze kulipa madeni hayo kwa awamu.

"Serikali inamatarajio makubwa kuona mnafanya kazi zenu kwa kuzingatia misingi ya sheria za utumishi wa umma na kanuni zake kwa kutumia taaluma zenu kutunza mali za umma hasa magari na miundombinu ya umeme kwani inagharimu fedha nyingi," alisema.

Mkurugenzi wa Matengenezo na Huduma za Ufundi, Mhandisi Hassan Koronda, alisema serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka na mwaka huu Sh. bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa karakara 12 katika mikoa mbalimbali ukiwamo Mkoa wa Singida ambao ujenzi wake wa awamu ya kwanza tayari umekamilika.

Aidha, Koronda alisema serikali imetoa Sh. milioni 509.8 kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya kisasa kwa upande wa umeme, ICT na mitambo kwa karakana za mikoa yote nchini kwa lengo la uboreshaji na utendaji wa kazi.

Mkuu wa Magari TEMESA Mkoa wa Singida, Erasto Cheza, akitoa taarifa ya mikakati ya utendaji wa kazi alisema wameondoa malalamiko yaliyokuwapo awali kwa kuyatambua na kuandaa mikakati ya kuyamaliza kwa kushirikiana na wadau wao.

Cheza alitaja majukumu yao ni kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya serikali, kufanya matengenezo na usimikaji wa mifumo ya umeme, mabarafu, viyoyozi na elektroniki.

Majukumu mengine ni kufanya matengenezo ya taa za kuongozea magari na taa za barabarani kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za uhandisi wa ufundi, umeme na elektroniki.



Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Gerald Mongela (kushoto), akizungumza na baadhi ya wadau wa maendeleo walipotembelea eneo la hospitali ya wilaya hiyo juzi, ili kuangalia uwezekano wa kusaidia ujenzi wa majengo mengine ya hospitali hiyo yenye eneo la ukubwa zaidi ya ekari 100. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Viongozi kata, mitaa wapewa maagizo kuhusu usafi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, amewataka viongozi wa mitaa na kata kusimamia usafi na kuwachukulia hatua za kisheria watakaokaidi ikiwamo kuwatoza faini kwa mujibu wa sheria ndogo ndogo za halmashauri za mwaka 2022.

Kimaro alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi habari jijini hapo kuhusu namna walivyojipanga kusimamia suala la usafi wa mazingira.

Alisema watendaji na wenyeviti hao washirikiane na polisi jamii na mgambo katika kuwatoza faini watakaobainika wanaharibu, kuchafua mazingira kwenye maeneo mbalimbali na kwa wale wote watakaokaidi kufanya usafi.

Aliwataka wasimamizi hao ngazi ya kata na mitaa kufanya ukaguzi katika maeneo yao na kuwachukulia hatua.

"Kila mtendaji wa kata ahakikishe watendaji wao wa ngazi ya chini wakiwamo na maofisa afya waliopo wanasimamia usafi wa kila siku na kwa wale ambao wanaoshindwa kutekeleza waripotiwe kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji,"alisema.

Kimaro aliwataka wafanyabiashara na wakazi wanaoishi kandokando mwa barabara kuu za Arusha, Iringa Dares-Salaam na Singida kushiriki uondoaji wa takataka kwenye maeneo hayo badala ya kusubiri kufanyiwa.

Pia aliviomba vikundi na kampuni za usafi kushiriki katika uondoaji wa taka ili kulifanya Jiji hilo kuendelea kuwa na mazingira yanayovutia na lenye usalama wa afya kwa upande wa Jiji.





# BRELA yawanoa wadau kuhusu sheria umiliki kampuni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), umeanza kutoa mafunzo maalumu kuhusu sheria ya umiliki wa kampuni ili kuwaepusha wadau na matatizo yanayoweza kuwapata ikiwamo utakatishaji wa fedha na uhujumu uchumi.

Mafunzo hayo yalitolewa jana jijini Mbeya kwa mara ya kwanza yakiwahusisha wadau mbalimbali wakiwamo mawakili, washauri wa biashara, wahasibu pamoja na wanafunzi wanaosomea fani hizo katika vyuo mbalimbali vya mkoa huo.

Mwakilishi wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Isdory Nkindi, alisema walianzisha mafunzo hayo baada ya mabadiliko ya sheria ya umiliki wa kampuni ambayo yalianza kuwatambua baadhi ya wadau ambao sheria na kanuni za awali zilikuwa haziwatambui.

Alisema baadhi ya wadau hao ambao ni wamiliki manufaa walikuwa hawaonekani kwenye nyaraka za usajili wa kampuni hali ambayo wakati mwingine walikuwa wanajikuta wanaingia kwenye matatizo ambayo walikuwa hawajui.

Alisema kwa sasa sheria inawataka wanufaika hao wa kampuni ambao awali walikuwa hawatambuliwi kusajiliwa kwenye daftari tofauti na wanufaika wengine.

"Lakini tumekuja huku kwa ajili ya kuwasikiliza wadau wetu wote wanaoshiriki kwenye urasimishaji wa biashara, tumekuja kuwasikiliza ili tujuwe matatizo ambayo wanakutana nayo kwenye kazi yao na tujadiliane namna ya kuzikabili," alisema Nkundi.

Ofisa Uhusiano wa BRELA, Roida Andusamile, alisema mafunzo hayo yanatolewa nchi nzima ili kuhakikisha wadau hao wanayafahamu mabadiliko ya sheria na kanuni zake na washiriki kwenye utekelezaji bila kukiuka taratibu.

Alisema baadhi ya kanuni zilizotungwa zinatakiwa kutekelezwa na wadau hao na hivyo ni muhimu wakazifahamu ili wanapotekeleza waepuke matatizo ambayo yamekuwa yakiibuka kupitia kwao bila wao wenyewe kujua. Alisema utekelezaji wa sheria na kanuni hizo utasaidia kulifanya taifa kuwa salama kwa kuepuka vitendo vya uhalifu ambavyo vimekuwa vikiibuka kupitia kwenye kampuni.

Roida alisema: "Hii itatusaidia kulifanya taifa letu kuepuka vitendo hivi vya uhalifu kama utakatishaji wa fedha na vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa vikisababishwa na kutotolewa taarifa sahihi za baadhi ya wamiliki hasa hawa wamiliki manufaa," alisema Roida.

Alisema wataendelea kutoa mafunzo hayo katika mikoa yote nchini ili kuhakikisha wadau wote wanakuwa na uelewa wa pamoja na kutekeleza vizuri sheria hiyo.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo waliwashukuru maofisa wa BRELA kwa kuwapatia mafunzo hayo wakieleza kuwa yatawasaidia kuepuka matatizo ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara.

Mmoja wa washiriki hao, Wakili Salum Kessy, alisema kabla ya mafunzo hayo walikuwa hawazijui baadhi ya kanuni mpya lakini baada ya mafunzo hayo watakuwa na uelewa wa kutosha.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kushiriki mpaka mwisho ili waelewe vizuri wanachofundishwa na watekeleze kwa vitendo kanuni hizo mpya.

Aliwapongeza BRELA kwa kuanzisha mafunzo hayo na kwamba yameanzisha muda ambao yametokea mabadiliko mbalimbali muhimu kwa maendeleo ya taifa.



Mkuu wa Sehemu ya Kampuni wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Isdor Nkindi, akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu uhamasishaji wa utekelezaji wa kanuni za wamiliki manufaa, baada ya ufunguzi wa kongamano la wadau mbalimbali mkoani Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRS yaadhimisha miaka 60 kuwapo Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Huduma za Misaada la Kikatoliki (CRS) limeadhimisha miaka 60 ya kuwapo Tanzania, huku likisisitiza kuendelea kujitolea kwa maendeleo ya binadamu kwa kukabiliana na dharura, maradhi na umaskini pamoja na kulea jamii zenye amani na uadilifu.

Mkurugenzi Mkuu wa CRS, Sean Callahan, alisema: "Wakati CRS duniani inatimiza miaka 80, ni heshima kubwa kuwapo Tanzania kwa miaka 60, tukifanya kazi bega kwa bega na Kanisa Katoliki la hapa nchini, washirika na jamii tunazohudumia na inaendelea kuwa jukumu kubwa kutokana na uaminifu tuliopewa".

Alisema CRS imekuwa ikihudumia Watanzania tangu mwaka 1962.

Alisema wakati ambapo mahitaji ya kibinadamu duniani yamefikia kiwango kikubwa, CRS inaendelea kuunga mkono mabadiliko yanayochochewa kwa kiwango kikubwa nchini kwa kufanya kazi bega kwa bega na viongozi wa dini mbalimbali, washirika wa kitaifa na jumuiya za wenyeji.

Katibu wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), Dk. Charles Kitima, katika maadhimisho hayo alisema uwepo wa mashirika kama hayo nchini kunasaidia kuwafundisha Watanzania kwenda kuwahudumia watu wengine wenye uhitaji.

Dk. Kitima aliishukuru serikali kwa kutoa msaada wa kibinadamu kwa nchi ya Malawi na Uturuki waliokumbwa na majanga ya kimbunga na tetemeko la ardhi.

Alisema katika kuunga mkono dhamira ya Wizara ya Afya ya kuhakikisha afya na ustawi wa wananchi katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona, CRS iliwezesha utoaji wa elimu na chanjo ya ugonjwa huo.

# Jeshi la Polisi lapokea msaada wa gari kukabili ajali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, imelikabidhi Jeshi la Polisi mkoani humo gari aina ya Toyota Harrier lenye thamani ya Sh. milioni 28 kwa ajili ya kuliwezesha kutekeleza vizuri majukumu yake hasa kukabiliana na tatizo la ajali za barabarani.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Rajabu Buliku alikabidhi gari hilo juzi kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, kwenye hafla iliyofanyika ofisi ya makao makuu ya polisi mkoa.

Alisema waliamua kutoa gari hilo kwa ajili ya kuliwezesha jeshi hilo hasa kikosi cha usalama barabarani kufanya shughuli za ukaguzi wa magari na vyombo vingine vya usafiri ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikisababisha vifo na majeruhi kwa wananchi.

Alisema kamati hiyo itaendelea kushirikiana na jeshi hilo kukabiliana na matatizo ya barabarani ili kuhakikisha matatizo ya ajali za barabarani yanapungua.

Alisema mbali na Jeshi la Polisi pia watashirikiana na wadau wengine wa usalama barabarani kukabiliana na ajali hasa kwa kutoa elimu kwa watumiaji wote wa barabara hasa madereva na wamiliki wa vyombo vya usafiri.

"Tunaamini kuwa gari hili litawasaidia wadau wetu hawa kutekeleza kwa ufanisi majukumu yao hasa ya kufanya doria za mara kwa mara kwenye barabara zetu ili kuwadhibiti madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani," alisema Buliku.

Akipokea gari hilo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kuzaga, aliishukuru kamati hiyo kwa kujitolea gari hilo akisisitiza kuwa itasaidia kushughulikia matatizo mbalimbali ya usalama barabarani.

Alisema uzinduzi wa kamati hiyo ni takwa la kisheria na ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya viongozi wakuu wa nchi waliyoyatoa katika maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama barabarani yaliyofanyika kitaifa jijini Mwanza.

Alisema kazi ya kamati hiyo ni pamoja na kushirikiana na Jeshi la Polisi kuzuia na kudhibiti ajali, kutoa elimu na kuwezesha vitendea kazi ambavyo vitarahisisha kazi ya askari wa kikosi cha usalama barabarani.

Alisema gari hilo litawasaidia maofisa wa jeshi hilo kufika maeneo mbalimbali na kutoa elimu, kufanya doria barabara kuu na maeneo tete.

"Tunawashukuru sana kwa kutusaidia kuboresha vitendeakazi, hapa tumekuwa tukihangaika wakati mwingine kuyafikia baadhi ya maeneo kwa sababu ya kukosa vitendeakazi, tunawaomba tuendelee kushirikiana," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka wadau wengine mkoani humo kuiga mfano wa kamati hiyo wa kulisaidia jeshi hilo kwenye shughuli mbalimbali za kukabili matukio ya uhalifu.

Alisema jeshi hilo liliamua kutumia mbinu ya kuyapitisha magari kwa awamu kwenye baadhi ya maeneo ya milima ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea.



# Vyombo vya habari vinavyokiuka maadili kudhibitiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Utangazaji Zanzibar imesema imejipanga kudhibiti vyombo vya habari hasa vya mtandaoni ambavyo vinakiuka maadili ya uandishi wa habari.

Akizungumza jana na Nipashe Ofisini kwake Mjini Zanzibar, Katibu Mtendaji wa tume hiyo, Suleiman Abdullah, alisema kuwa mwitikio wa vijana kwenye kujiajiri na kutanua fursa za kitaaluma kupitia mitandao ya kijamii ni kubwa.

Alisema Zanzibar kuna televisheni za mitandaoni 63, hivyo ni vyema wamiliki wa vyombo hivyo kuhakikisha wanafuata maadili ya taaluma ya uandishi wa habari.

Katibu huyo alisema tume imeshapokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu baadhi ya mitandao hiyo ambayo inakiuka taratibu za uandishi wa habari kutokana na taarifa zinazotolewa katika mitandao hiyo.

"Hivi karibuni tumepokea malalamiko kutoka kwa familia moja ambayo baba yao kahusishwa na familia ya afande Rama anayetuhumiwa kufanya mapenzi ya jinsia moja wakati mzee huyo hana uhusiano wowote na mtuhumiwa huyo,"alisema.

Aidha, alisema lazima vyombo hivyo vizingatie maslahi ya taifa na kuhakikisha wamiliki wake wanajisajili katika tume hiyo ili kuepuka kufungiwa.

"Tunawapa fursa vijana wenye taaluma ya habari na wale wasio na taaluma hiyo lakini wanataka kuanzisha televisheni hizo za mtandaoni tunawaelekeza namna ya kufanya kazi kwa kuzingatia taratibu za kiserikali,"alisema.

Alisema tume hiyo inafuatilia taarifa zote zinatolewa na televisheni hizo za mtandao ili kuhakikisha mitandao hiyo haikiuki maadili na pale inapokiuka hufuatiliwa na kupewa adhabu stahiki kwa mujibu wa sheria.

Naye Mkurugenzi wa asasi ya kiraia inayoshughulikia masuala ya vijana iitwayo Zanzibar Youth Forum, Maulid Suleiman aliwataka vijana kuitumia vizuri fursa ya uwepo wa mitandao ya kijamii kwa lengo la kujitafutia ajira na kukuza uchumi.




Balozi wa Kampuni ya Vigor Zanzibar, Haitham Salum Turkey (katikati), akizungumza na watendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, jijini Zanzibar jana, baada ya kampuni hiyo, kukabidhi vyakula kwa ajili ya matumizi ya hospitali. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mipango wa hospitali hiyo, Abdallah Kahmis Haji. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanawake wenye nia ya kugombea uongozi wafundwa

**Na Mwandishi Wetu** PEMBA

KATIKA kuhakikisha lengo la ushiriki sawa wa wanawake kwenye nafasi za uongozi linafikiwa, wanawake wenye nia ya kugombea na kushika nafasi hizo wametakiwa kubaini matatizo yanayowakabili na kuyatatua badala ya kusubiri kipindi cha uchaguzi.

Hayo yalielezwa na wadau wa usawa wa kijinsia wakati wa mafunzo maalumu ya kuwajengea uwezo wanawake 35 wenye dhamira ya kugombea kutoka vyama mbalimbali vya siasa Kisiwani Pemba yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, (TAMWA- Zanzibar) kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway kutambua misingi, taratibu, wajibu na hatua muhimu za kufuatwa kabla na wakati wa kugombea ili kuwa kiongozi bora katika jamii.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Dk. Salum Suleiman Ali, kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) alisema wanawake wananguvu ya ushawishi na iwapo watajua namna ya kuitumia kwa kujenga hoja na kuwa karibu na jamii itawasaidia kufikia malengo na kushika nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali bila vikwazo.

"Wanawake lazima kwanza tuwe na uwezo wa kujitayarisha kiuongozi ikiwamo kuyaacha baadhi ya mambo ambayo yanaweza kutumika kukuboмoa. Kisha utambue matatizo yaliyopo katika jamii na kubaini fursa zilizopo za kuweza kutatua," alieleza Dk. Salum.

Aidha, alisema ili kufikia lengo hilo kila mwanamke anatakiwa kuwa jeshi la kumlinda na kumwongoza mwenzake kwenye masuala ya uongozi ili kujenga heshima ya wanawake wote kwenye uongozi bila kuharibu heshima ya wanawake wengine.

Alisema: "Mafunzo haya yamekuja mapema ambapo bado miaka miwili kuelekea uchaguzi mkuu kwasababu kuna mambo muhimu unatakiwa kuyaanza mapema na siyo kusubiri uchaguzi umefika ndipo uanze mchakato kwasababu kwenye siasa siyo ujanja bali ni mikakati bora inayolenga kutetea wananchi unaowaongoza."

Mratibu wa TAMWA-Zanzibar kutoka Pemba, Fat-hiya Mussa Said aliwataka wanawake kushikamana bila kujali tofauti za vyama vya siasa, lengo likiwa ni kufanikisha kupata idadi kubwa ya wanawake wanaoingia katika nafasi za uongozi.

Mkurugenzi wa Jumuiya ya Utetezi wa Jinsia na Mazingira Pemba (PEGAO), Hasjim Abdi Said, akizungumzia kuhusu mafunzo hayo yaliyoandaliwa kupitia mradi wa wanawake na uongozi alisema yanalenga kuwaandaa wanawake weye nia ya kugombea nafasi hizo kuwa na uwezo wa kusimama kutatua changamoto zinazoikabili jamii kabla ya kugombea katika chaguzi mbalimbali.

Mmoja wa washiriki kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Pemba, Zainab Mussa Bakar, aliwataka wanawake wenye nia ya kugombea nafasi za uongozi kuwekeza nguvu katika kujijengea uwezo binafsi ikiwemo kujiendeleza kielimu ili kuepukana na changamoto za udhalilishaji wanazokumbana nazo kipindi cha uchaguzi.

# Wananchi watakiwa kuwafichua watumishi wapenda rushwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amewataka wananchi kutoa ushirikiano wa kuwafichua baadhi ya watumishi wa umma wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

Haroun ambaye ni Mwakilishi wa Makunduchi, aliyasema hayo jana katika kikao cha pamoja kati ya watendaji kutoka sekta za serikali pamoja na wananchi kwa lengo la kuzungumzia changamoto zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi.

Alisema suala la uchukuaji wa rushwa kwa watumishi hasa katika chombo cha Mahakama kinachotoa haki za watu halikubaliki na ni kwenda kinyume na maadili yao ya kazi.

Waziri Haroun alifahamisha kuwa hali hiyo inasababisha kuwapo kwa manung'uniko mengi kwa wananchi pale wanapokwenda kudai haki zao kushindwa kuzipata.

Aidha, alisema serikali itawachukulia hatua watumishi watakaobainika wanajihusisha na vitendo hivyo ambavyo vinakwenda kinyume na sheria na taratibu za utumishi wa umma.

Ame Juma miongoni mwa wananchi hao alisema suala hilo linawavunja moyo na kuwaweka katika wakati mgumu kutokana na wengi wao wanaofika kudai haki zao hasa mahakamani uwezo wao mdogo na linarudisha nyuma jitihada za serikali katika kutoa huduma bora za maendeleo ya kijamii.

Wakizungumzia kero zao mbalimbali zinazowakabili walisema ni pamoja na uhaba wa dawa, umeme mdogo na ukosefu wa uzio katika Hospitali ya Wilaya Makunduchi.

Akizungumzia kuhusu masuala ya umiliki wa maeneo ya ardhi Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, aliwataka wananchi kulipa umuhimu suala la utafutaji wa hati za umiliki wa ardhi kisheria ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LATIFA SHABANI MASOUD** anatangaza kupotelewa na Living Certificate pamoja na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2761/0068** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KEREZANGE SEKONDARI** mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHA/RB/113149/2023.**

---

**IN THE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 34 of 2023**

**In the matter of application for letters of administration by EVARISTO JOHN CHALLO AND BUMI MWAISAKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 20 day of 04/2023

Dated at Dodoma this 28 day of March 2023

---

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No.27 of 2023**

**In the matter of the Estate of the late of the late NOEL MICHAEL KIGOLA**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by MICHAEL SULTAN KIGOLA.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 5 Day of 4, 2023

Dated at Dodoma this **30 day of 3, 2023**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

**SHAURI LA MAOMBI LA ARDHI NA.88 YA 2022**

**PATSON SHUNGU...............................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**CASTONE JIMSON NA WENZAKE 3......WAJIBU MAOMBI**

**KWA; 1. Castone Jimson,**
**2. God Christopher Mpangala,**
**3, Tumain Mpangala,**
**4, Munya Mbuya,**

**POPOTE MLIPO.**

**KUITWA SHAURINI.**

Mnaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama kuu kanda ya Mbeya tarehe 3/5/2023 siku ya Ijumaa saa 3.00 asubuhi ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
Eleweni kwamba,mkikosa kufika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja bila ninyi kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 16 Februari 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 30 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE GOODLUCK AINEA MCHAU AND IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SUZANA GOODLUCK MCHAU**

**GENERAL CITATION**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 05 Day of 05, 2023

**Dated at Dodoma this 03 day of March, 2023**

PETITIONER

RESIDENT MAGISTRATE

**Presented for filling this 30 Day of March 2023**

---

## MNADA WA HADHARA

**RAISSA COMPANY LIMITED** tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana ya mdaiwa sugu kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.Mnada utaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd** kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| BISWARO ZEBEDAYO MSASE | Nyumba- iliyopo Mloganzila- Kwembe - Dsm | 14/04/2023 |

**MASHARTI MENGINE:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena.

Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: RAISSA Company Ltd: 0652113262/ 0757433333**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TITUS ROBERT RWEYEMAMU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **SM 4430.** Chassis No. **JTECB09J603026230.** Engine No. **IHZ0503996.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/115622/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IBRAHIM ALBERT KOMU** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 380 CSG.** Chassis Namba **TZ50002586,** Engine Namba **QR25234216A** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taafifa: **KIL/MOS/RB/115190/2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.24 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late GLADIS WILLIAM NGALAI**
**Of Dodoma Municipal – Dodoma City**

**AND**

**In the matter of an application for letters of administration by ALANI NOEL DAUDI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner thereof.

Objections to the grant should be filed on or before the **5 Day of 4, 2023**

Dated at Dodoma this **30 day of 3, 2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na 256/2022**
**Jina la Mdai DEVOTA MATHEW MINJA**
**Jina la Mdaiwa JACKSON SHIRIMA**
**AMRI YA KUUZA MALI KUTIMIZA HUKUMU**

**(Kanuni ya 72, 73 & 78 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ROYAL RUNNERS & GENERAL SUPPLIES S.L.P 10485 DODOMA**

**K.K Kwa Hakimu Mkazi Mfawidhi**
**Wilaya DODOMA MAHAKAMA YA MWANZO**

Kwa hati hii nakuamuru kuuza katika Mnada wa Hadhara baada ya kutangaza kwa muda wa siku 21 kwa kubandika katika mbao za matangazo na Nyumba ya mdeni Mhukumiwa ikieleza wakati na mahala patakapo fanywa mnada huu na mali itakayouzwa, na baada ya kutangaza mali ambayo ni GARI NO T.158 CDN iliyokamatwa kwa hati ya kukamatia mali iliyotolewa na Mahakama hii tarehe 23 Mwezi 2 Mwaka 2023 kwa kutimiza hukumu ya mdai alietajwa hapo juu, au mali itakayokamilisha kiasi cha shilling 8,000,000 Unaamriwa tena kurudisha hati hii kabla ya tarehe 4 Mwezi 4 Mwaka 2023 ikiwa na maandishi yako ya kuthibitisha namna amri ilivyotekelezwa au kwanini haikutekelezwa.
Endapo mdeni mhukumiwa atalipa na kuthibitisha kiasi kinachodaiwa na gharama zote za mnada kabla ya tarehe ya mnada, mnada wa mauzop utasitishwa.
ORODHA YA MALI INAYOTAKIWA KUUZWA
GARI AINA YA FUSO NO T.158 CDN
Amri na Muhuri wa Mahakama leo tarehe 15 Mwezi 3 Mwaka 2023

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB:**
**+255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Maandamano yaivuruga Kenya

**NAIROBI,** Kenya

MAANDAMANO ya raia wa Kenya kupinga hali ngumu ya maisha yameendelea jana na kuvuruga shughuli za kibiashara katika mji mkuu wa Nairobi.

Jeshi la Polisi liliweka ulinzi mkali katika jiji la Nairobi, baada ya serikali kupiga marufuku maandamano ya upinzani ambayo yamepangwa kufanyika kila Jumatatu na Alhamisi.

Vyombo vya habari vya ndani vimekuwa vikiripoti maandamano hayo katika kaunti mbalimbali nchini humo.

**Polisi waliweka vizuizi vya barabarani katika barabara kuu na zile zinazoelekea Ikulu ya Rais Willium Ruto.**

Polisi walitumia mabomu ya machozi kuwatawanya waandamanaji katika ngome za upinzani kwenye maeneo yanayoaminika kuwa ngome ya wapinzani.

Aidha, polisi waliweka vizuizi vya barabarani katika barabara kuu na zile zinazoelekea Ikulu ya Rais Willium Ruto.

Mamlaka, hata hivyo, zimesitisha huduma za treni jijini Nairobi kabla ya maandamano hayo kuanza.

Waandamanaji katika miji ya magharibi ya Kisumu, Homa Bay na Migori tayari walifunga barabara kwa kuchoma moto matairi ya magari na mawe makubwa.

Naibu Rais Rigathi Gachagua, alifika ofisini mwake alfajiri na aliwataka Wakenya kwenda katika maeneo yao ya kazi na kupuuza maandamano hayo.

**KUZUIA MACHAFUKO**

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Kenya imesema nchi hiyo iko kwenye ukingo wa machafuko, hali ambayo ni hatari kubwa kwa utawala wa sheria na uthabiti wa nchi yetu.

Kulingana na wizara hiyo, iliapa kupeleka polisi wa kutosha ili kukomesha kile ilichokiita kushuka kwa machafuko yasiyoweza kurejeshwa.

Raila Odinga ameitisha maandamano mara mbili kwa wiki, Jumatatu na Alhamisi, kupinga kupanda kwa gharama ya maisha na kupata haki baada ya uchaguzi wa mwaka jana.

Takriban watu wawili wameuawa katika maandamano hayo, huku raia 85 na maofisa wa polisi 51 walijeruhiwa, kulingana na wizara hiyo. **BBC**



Waandamanaji waliokusanyika jana eneo la mabanda jijini Nairobi katika mwendelezo wa maandamano yaliyoitishwa na kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga kwa ajili ya kuipinga serikali. **PICHA: AFP**

## UN yalaani vikali ghasia DR Congo

**NEW YORK,** Marekani

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa, limelaani vikali ghasia zinazofanywa na makundi yenye silaha mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kuwataka wanamgambo hao kuweka chini silaha.

Kwenye kikao maalumu kwa ajili ya DRC, kilichofanyika usiku wa kuamkia jana, mabalozi wa nchi wanachama wa baraza hilo wamelaani vikali kuendelea kwa ghasia na ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na wapiganaji kwenye majimbo ya Kivu Kaskazini, Ituri na Kivu ya Kusini.

Baraza la Usalama limeyataka pia makundi yenye silaha kujisambaratisha mara moja, kuweka chini silaha na kuwaachilia watoto kutoka kwenye makundi hayo.

Nicolas De Rivière, balozi wa Ufaransa kwenye Umoja wa Mataifa, alisema wanawasiwasi mkubwa kuhusu kuzorota kwa usalama mashariki mwa DRC.

"Tunaendelea kuhuzunishwa kuenea kwa unyanyasaji wa kijinsia unaohusiana na migogoro. Ghasia hizo mara nyingi hutumika kama mbinu ya vita yenye athari kubwa kwa wahanga, familia na jamii zao. Tunahimiza mamlaka za DRC kuendeleza juhudi zao za kukomesha mzunguko wa kutoadhibiwa kwa uhalifu huu, alisema De Rivière.

Kwenye taarifa yao, mabalozi hao wa baraza la usalama la Umoja wa Mataifa walilenga hasa kundi la M23, ambalo mashambulizi yake yameongezeka katika miezi ya hivi karibuni huko Kivu Kaskazini.

Akihutubia baraza la usalama, Mkuu wa kikosi cha kulinda amani cha umoja wa mataifa nchini DRC, Bintou Keita alisema hali ya kibinadmu mashariki mwa nchi hiyo inatia wasiwasi.

"Kuongezeka kwa mzozo wa kundi la M23 na kuendelea kwa shughuli za vikundi vingine vyenye silaha, vikiwamo ADF, Zaire na CODECO, kunaendelea kusababisha mateso makubwa kwa raia na kuzidisha hali mbaya ya kibinadamu, ambayo inazidi kuwa janga," alionya Bintou. **BBC**

## Ukraine yaingia mgogoro na kanisa

**KYIV,** Ukraine

MAKASISI wa Kanisa la Othodox nchini Ukraine, wanasema watasalia katika makao ya watawa ya kihistoria katika mji mkuu wa Kyiv.

Kauli ya viongozi hao ya kidini inatokana na mpango wa serikali wa kuwaondoa mamia ya makasisi, watawa na wanafunzi.

Pechersk Lavra ni makao makuu ya Kanisa la Orthodox la Ukraine (UOC), ambalo lilijitenga na mfumo dume wa Russia baada ya uvamizi mwaka jana.

Hata hivyo, maofisa wa Ukraine wanashuku baadhi ya makasisi wakuu wamedumisha uhusiano na Kanisa hilo nchini Russia, jambo ambalo wanalikanusha.

UOC iliamriwa kuondoka kufikia mwisho wa Jumatano.

Serikali ya Ukraine, ambayo inamiliki monasteri kubwa ya Karne ya 11 inayotazamana na mto Dnipro, ilisema uamuzi huo ulichukuliwa baada ya tume kugundua ukiukwaji mwingi wa makubaliano ya upangaji wa majengo hayo, eneo la Urithi wa Dunia wa UNESCO.

Metropolitan Clement, mkuu wa ofisi ya waandishi wa habari ya UOC, alisema hakuna msingi wa kisheria wa kufukuzwa, uliotangazwa mapema mwezi huu.

"Ikiwa serikali inatulazimisha kufanya hivyo kinyume cha sheria, inaitwa uimla," aliambia BBC.

"Hatuhitaji serikali kama hiyo. Tuna katiba na sheria. Hatukubali mbinu zingine." Alisisitiza.

Mamlaka ya Ukraine inawashutumu baadhi ya wanachama wa UOC kwa kuunga mkono Russia kwa siri wakati wa vita, ingawa baadhi ya viongozi wameshutumu uvamizi huo.

Mwaka jana, idara ya usalama ya Ukraine ilifanya uvamizi huko Lavra na majengo mengine ya UOC, na kuwakamata makasisi kwa tuhuma za uhaini na ushirikiano na Russia. **BBC**

## Papa alazwa hospitalini

**ROMA,** Vatcan

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, ameendelea kulazwa hospitalini baada ya kupata changamoto ya upumuaji.

Taarifa kutoka ndani ya kanisa hilo mjini Roma, inaeleza kiongozi huyo atahitaji kukaa kwa siku chache hospitalini kwa ajili ya uangalizi wa karibu.

Papa Francis mwenye umri wa miaka 86, alikuwa na shida ya kupumua katika siku za hivi karibuni lakini hana Covid 19, taarifa hiyo ilisema.

"Papa Francis ameguswa na jumbe nyingi alizopokea na anatoa shukrani zake kwa ukaribu na sala," iliongeza taarifa hiyo.

Ofisa mmoja alisema, wafanyakazi wake wa karibu, wakiwamo wa usalama, wanatarajiwa kulala katika Hospitali ya Gemelli.

Kipindi hiki ni muhimu kwa Papa Francis, hasa matukio na ibada nyingi zikipangwa kabla ya wiki ya Pasaka.

Misa ya Jumapili ya Mitende imepangwa mwishoni mwa wiki ikifuatiwa na maadhimisho ya wiki Takatifu ya Pasaka.

Siku ya Jumatano asubuhi, aliongoza hadhira yake ya jumla ya kila wiki katika Uwanja wa Mtakatifu Peters. Alionekana mwenye huzuni huku akisaidiwa kuingia kwenye gari lake.

Awali Vatican ilisema Papa alienda hospitalini kwa uchunguzi uliokuwa umepangwa awali, lakini vyombo vya habari vya Italia vimetilia shaka maelezo hayo baada ya mahojiano ya televisheni kufutwa kwa taarifa fupi. **BBC**

# SERIKALI YATANGAZA KUNUNUA JENERETA MPYA 2 KWA MKAPA

**Na Saada Akida**

SERIKALI imesema ipo katika mchakato wa kuuboresha Uwanja wa Benjamin Mkapa ulioko Dar es Salaam pamoja na kununua jenereta mbili zenye uwezo mkubwa wa kuwasha taa endapo kutakuwa na changamoto ya kukatika umeme, imeelezwa.

**Taarifa hiyo imekuja siku chache baada ya mechi kati ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) dhidi ya Uganda kusimama kwa zaidi ya dakika 30 kutokana na jenereta lililokuwapo kushindwa kuwasha taa na kuleta sintofahamu.**

Akizungumza jijini jana, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, alisema kwa sasa wameshaanza mchakato wa kuboresha uwanja huo ili kuwa wa kisasa kama vilivyo viwanja vya nchi zilizoendelea.

Chana alisema pia serikali iko katika mchakato wa kuboresha viwanja vilivyoko katika mikoa ya Mbeya, Tanga, Dodoma na Arusha ili kuhakikisha wanakuwa na viwanja bora zaidi vya michezo.

"Tuko na mikakati ya kuboresha uwanja wetu wa Benjamin Mkapa kuwa bora zaidi ya sasa, baadhi ya viwanja mikoani na kujenga viwanja vya mazoezi katika eneo la Kawe," alisema Chana.

Waziri huyo alisema pia serikali inaangalia changamoto mbalimbali zinazowakuta wanamichezo ikiwamo suala la mikataba ya wachezaji na ufanisi wa viongozi kuhakikisha michezo inazidi kufanya vizuri.

"Suala la mikataba ya wachezaji litasimamiwa kwa umakini na kuweka mikakati ya nyota hao kupata haki zao za msingi, kulipwa vizuri lakini pia timu zinatakiwa kufanya vizuri katika michuano iliyopo mbele yao kama ilivyo kwa Simba na Yanga," Chana alisema.

Aliongeza wanajipanga kuona sekta ya michezo Tanzania inakua kwa kasi lakini pia kuboresha kwenye utamaduni kwa kuzungumza na taasisi na benki mbalimbali kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wasanii.

Naye Katibu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema changamoto kubwa inayofanya michezo kutosonga mbele hapa nchini ni kukosekana kwa miundombinu bora ikiwamo viwanja vya kisasa.

Kidao alisema Tanzania haina viwanja vya kutosha ambavyo ni bora kwa ajili ya kumfundisha mtoto kuanzia umri wa chini na timu za ligi kutokuwa na viwanja wa mazoezi ambavyo vinamilikiwa na klabu hizo ni tatizo lingine.

"Lazima mtoto anatakiwa kujifunza katika kiwanja bora kwa kuanza kufundishwa mpira, lakini pia kuwapo kwa sera nzuri katika michezo shuleni kama ilivyokuwa zamani tulipokuwa tukisoma na kupata nafasi ya kufanya michezo shuleni," alisema Kidao.



Aliyekuwa kocha wa makipa wa Simba, Mohammed Muharami (kushoto), akitoka katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam jana baada ya kesi yake ya kutuhumiwa kusafirisha dawa za kulevya inayomkabili yeye na wenzake kuahirishwa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# *Rekodi za JKT Tanzania zafunika*

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuongoza kwa kukusanya pointi 56 katika Ligi ya Championship na kukaribia kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, timu ya JKT Tanzania imeweka rekodi kadhaa nzuri ikiwamo kuongoza kushinda mechi nyingi ugenini na nyumbani.

Kwa mujibu wa takwimu za ligi hiyo, JKT Tanzania ambao wameshacheza mechi 23, wakisalia na mechi saba tu wameshinda mara 10 nyumbani kati ya mechi 12 huku wakishinda michezo nane ugenini kati ya mechi 11 ambazo wameshuka dimbani.

Wakati Maafande hao wakiwa vinara katika ligi hiyo, na kushinda mechi nyingi za nyumbani na ugenini, Kitayoce ya Tabora ambayo inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 49, inaifuatia JKT Tanzania kwa kushinda mechi nyingi nyumbani, imeshinda mara tisa kati ya michezo 11.

Pamba inashika nafasi ya tatu kwa pointi zake 47, inashika nafasi ya pili kwa timu zilizoshinda mechi nyingi ugenini, ikifanya hivyo mara saba kwa michezo 12 iliyocheza.

Takwimu hizo inaonyesha nafasi ya tatu kwa timu zilizoshinda nyumbani inashikiliwa na Mashujaa, ikishinda mara tisa kati ya mechi 12, Pamba wako katika nafasi ya nne wakicheza mechi 10 na kushinda nane huku KenGold wakimaliza tano bora kwa kushinda mechi nane.

Mbuni FC iko katika nafasi ya sita ikishinda mechi nane nyumbani kwa michezo 12 iliyocheza.

# Meridian waja na dozi juu ya dozi

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Meridianbet umesema umekuja na 'dozi juu ya dozi' kwa ajili ya kurejesha dau kwa shabiki ambaye amechana mkeka au tiketi kila siku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet, Matina Nkurlu, alisema kampuni hiyo imekuja na Jakipoti kubwa ya mechi 13 kwa dau dogo la kuanzia Sh. 1,000 na mshindi atajinyakulia donge nono.

Nkurlu alisema wamekuja na promosheni nyingine ambayo si ya kinyonge, inampa shabiki nafasi ya kuwa mshindi wa kila siku hata kama 'amechana' na timu moja.

"Tunatoa Cash Back mpaka mara 100 ya dau ulilowekа. Habari njema zikufikie popote ulipo mdau wa kubashiri na Meridianbet kwa kuwa unapata odds kubwa, machaguo zaidi ya 1000+ na Ofa za kumwaga," alisema na aliongeza;

Hii nyingine ya kijanja zaidi unaambiwa usijali endapo mkeka wako utachanika kwa timu moja, Meridianbet mkeka bado umeshinda kwa sababu wanakurudishia mara 100 ya dau lako ulilowekа," alisema Nkurlu.

Aliongeza kitu anachotakiwa kufanya shabiki ni kubashiri tiketi yenye odds kubwa kuanzia 25+ hadi 950 +, ambazo utarejeshewa mara 100 ya dau ambalo limetolewa kama ikitokea timu moja imechana mkeka huo.

"Tiketi haitakiwi kuwa na bashiri ya mechi moja tu, unatakiwa uwe na angalau bashiri moja kutoka bashiri za kabla ya mechi, haitakiwa kuweka machaguo mengi (Mult-bet) kutoka mechi moja.

Hii ni maalumu kwa tiketi zilizopoteza mechi moja na dau la bonasi halihusiki kwenye promosheni hii, kupata jumla ya ushindi zidisha jumla ya odds zilizoshinda pekee (Odds za bonasi hazihesabiwi), halafu zidisha kwa namba zilizoainishwa katika jedwali hapo kulingana na idadi ya mechi kwenye tiketi yako," alisema Nkurlu.

Mkuu huyo wa alisema pia odds kubwa zilizoshinda hazihusishi ongezeko la odds za bonasi.

**Tunatoa Cash Back mpaka mara 100 ya dau ulilowekа. Habari njema zikufikie popote ulipo mdau wa kubashiri na Meridianbet kwa kuwa unapata odds kubwa, machaguo zaidi ya 1000+ na Ofa za kumwaga.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE AGEUKA LULU

KIUNGO wa kati wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, ndiye mchezaji anayesakwa zaidi na Arsenal msimu huu wa joto na kuna imani inayoongezeka wanaweza kufanikiwa kuwashinda Chelsea, Manchester City na Manchester United ili kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England. ***(Evening Standard)***

### MADRID YAPANIA USAJILI

REAL Madrid imemfanya kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19 kuwa usajili wao wa kipaumbele. Hata hivyo miamba hao wa Hispania pia wanavutiwa na mlinzi wa Chelsea, Reece James (23). ***(AS)***

### UNITED YAMTAJA MUANI

MANCHESTER United inamfuatilia mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt na Ufaransa, Randal Kolo Muani mwenye umri wa miaka 24 pamoja na straika wa Atalanta na Denmark, Rasmus Hojlund (20), iwapo wataambiwa bei kubwa kwa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane (29). ***(Manchester Evening News)***

### UNITED KUMKOSA SABITZER

MANCHESTER United huenda ikakosa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Austria, Marcel Sabitzer, 29, kwa usajili wa kudumu baada ya mkataba wake wa mkopo kumalizika huku kocha mpya wa Bayern Munich, Thomas Tuchel akiamua kumbakisha mchezaji huyo. ***(Sun)***

### POCHETTINO ANUKIA SPURS

KOCHA Julian Nagelsmann, 35 na Mauricio Pochettino (51), wako tayari kurithi mikoba ya Antonio Conte katika klabu ya Tottenham Hotspur - hata hivyo wote wawili watasubiri kuona kama kibarua cha Real Madrid kitapatikana katika msimu wa joto. ***(90min)***

### ENRIQUE AITAMANI EPL

KOCHA wa zamani wa Hispania, Luis Enrique, 52, amesema angependa kufundisha katika Ligi Kuu England maarufu EPL, katika timu ambayo inaweza kufanya "mambo makubwa". ***(Cadena SER)***

### GUNDOGAN KUTUA BARCA

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, 32, yuko tayari kuondoka Manchester City na kujiunga na Barcelona kwa uhamisho wa bure mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Insider)***

### BARCA YAMWINDA GUNDOGAN

BARCELONA itaendeleza mpango wa kumnunua, Ilkay Gundogan, baada ya kufikia makubaliano ya mdomo kumsajili beki wa kati wa Athletic Bilbao ambaye ni raia wa Hispania, Inigo Martinez, 31. ***(ESPN)***

### BARCA, ARSENAL VITANI

BARCELONA itakabiliana na ushindani kutoka kwa Arsenal na Chelsea katika mbio za kumnunua mshambuliaji wa Athletico Paranaense na Timu ya Taifa ya Brazil, Vitor Roque, 18. ***(Sport)***

### VUSKOVIC AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Manchester City na Paris St-Germain zimewasilisha ombi la kwanza kwa mlinzi wa Hajduk Split kutoka Croatia, Luka Vuskovic, 16. ***(90min)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD: SIJASHINIKIZA KULIPWA MSHAHARA MNONO

**●●● Asema tetesi hizo ni upuuzi kwa sasa anawaza kuona wanashinda...**

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford amekanusha na kuita "upuuzi" ripoti anataka mkataba mpya utakaomfanya alipwe mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki ili kubakia Manchester United.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa England ambaye amefunga mabao 27 katika michezo 44 msimu huu, anatarajia kumalizika mkataba wake hapo Old Trafford mwishoni mwa msimu ujao.**

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Star, mustakabali wa Rashford hapo United uko katika sintofahamu kutokana na mauzo yanayoendelea ya klabu hiyo na madai yake makubwa ya mshahara.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alikanusha kuhusu bahari hiyo kupitia kwenye ukurasa wake wa Twitter kwa kuandika sio kweli.

"Ni upuuzi mtupu," aliandika.

"Lengo langu ni kumaliza vizuri iwezekanavyo kwenye ligi na kushinda mataji."

Rashford aliongeza katika Instagram: "Hii sio sawa kabisa. Ni upuuzi mtupu!

"Lengo langu na malengo ya klabu ni kumaliza juu iwezekanavyo kwenye ligi na kujaribu kushinda taji moja au mataji mawili."

Rashford ametumia misimu nane kama sehemu ya kikosi cha kwanza cha United tangu aanze kwa mafanikio makubwa akiwa na mabao mawili kwenye mechi yake ya kwanza dhidi ya Midtjylland Februari, mwaka 2016 akiwa na umri wa miaka 18.

Akizungumza mwezi uliopita, Kocha wa United, Erik ten Hag, alithibitisha klabu hiyo inajitahidi kuwapa mikataba mipya wachezaji wao walitokea kwenye akademi yao.

"Bila shaka mkataba mpya wa Rashford ni kipaumbele," alisema. "Tunafanyia kazi hilo."

Rashford alikosa mechi mbili za England za kufuzu Euro 2024 kutokana na majeruhi, lakini anatarajiwa kuwa fiti kucheza dhidi ya Newcastle United Jumapili.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,096,0
MECHI KALI
BURNLEY
VERSUS
SUNDERLAND
1 | 1.44
X | 4.29
2 | 6.19
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ENRIQUE AITAMANI EPL



**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Hispania na Barcelona, Luis Enrique, anataka kufanya kazi katika Ligi Kuu England, lakini amekataa kuchukua nafasi ya Antonio Conte pale Tottenham Hotspur.

Enrique aliachana na Hispania baada ya Kombe la Dunia la 2022, ambalo La Roja hao walitolewa na Morocco katika hatua ya 16 bora.

Nafasi yake ilichukuliwa na Luis de la Fuente, ambaye alitoka kwenye Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 21.

Watu wanaohusishwa na kazi za kiwango cha juu wamekuwa mara kwa mara tangu wakati huo, lakini klabu anayoonekana kuhusishwa nayo zaidi ni Spurs, ambao Jumapili iliyopita walimfukuza Conte baada ya wiki ya uvumi mkubwa wakidai muda wake umekwisha.

Ingawa Enrique hakuulizwa moja kwa moja kuhusu Spurs wakati wa mahojiano yake, alielezea nia yake ya kufanya kazi kwenye Ligi Kuu England.

"Ningependa kwenda kufanya kazi England," aliiambia redio SER Gijon.

"Lakini sijioni kwenye Ligi Kuu mnamo Julai kwa sababu ningependa kwenda kwenye timu ambayo inaweza kufanya mambo muhimu, na hiyo ni ngumu sana.



# Madrid kumchukua James

**MADRID,** Hispania

CHELSEA hawajaimarika msimu huu na wanaweza kuwaondoa wachezaji ili kuhakikisha wanakidhi mahitaji ya kucheza kwa usawa wa kifedha, na kuna uwezekano, Reece James akaondoka hapo Stamford Bridge.

The Blues wametumia fedha nyingi katika kipindi cha miezi 10 tangu Todd Boehly achukue umiliki kutoka kwa Roman Abramovich.

Enzo Fernandez, Wesley Fofana, Mykhailo Mudryk, Marc Cucurella, Raheem Sterling, Benoit Badiashile, Kalidou Koulibaly, Noni Madueke na Malo Gusto wote walisajiliwa hivi karibuni.

Na sasa Real Madrid wanapanga kumsajili beki wa pembeni wa Chelsea, James, kwa mujibu wa AS.

James mwenye umri wa miaka 23 ana mkataba na The Blues hao hadi mwaka 2028, na kufanya mpango wowote kuw mgumu, lakini Los Bla cos wanaripotiwa na m tumaini ya kumchukua

Hapo awali Madrid i wapata Thibaut Courtc na Eden Hazard kutol Chelsea, ingawa kati mazingira tofauti hul wote wakiwa wamebal wa na muda mfupi kati mikataba yao ya sasa.

AS imeripoti kiung wa Borussia Dortmun Jude Bellingham, anab kia mchezaji anayepew kipaumbele na Madrid.

## HABARI MICHEZO


041,286/-

# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII
## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/04/23 | 17:00 | AFC Bournemouth vs Fulham FC | 2.45 | 3.10 | 2.80 |
| 02. 01/04/23 | 17:00 | Crystal Palace vs Leicester City | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 01/04/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Wolverhampton Wanderers | 2.85 | 3.00 | 2.45 |
| 04. 01/04/23 | 19:30 | Cadiz CF vs Sevilla FC | 3.05 | 3.00 | 2.33 |
| 05. 01/04/23 | 21:00 | SC Cambuur vs FC Emmen | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 01/04/23 | 22:00 | RKC Waalwijk vs Vitesse Arnhem | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 07. 01/04/23 | 22:00 | Stade Rennes vs RC Lens | 2.36 | 3.25 | 2.80 |
| 08. 02/04/23 | 13:30 | Bologna FC vs Udinese Calcio | 2.23 | 3.15 | 3.10 |
| 09. 02/04/23 | 13:30 | Umraniyespor vs Konyaspor | 2.90 | 3.50 | 2.24 |
| 10. 02/04/23 | 15:15 | Grasshopper Club Zurich vs FC Lugano | 2.47 | 3.15 | 2.41 |
| 11. 02/04/23 | 16:00 | FC Nantes vs Stade Reims | 2.90 | 3.20 | 2.33 |
| 12. 02/04/23 | 16:00 | Stade Brest 29 vs Toulouse FC | 2.80 | 3.30 | 2.34 |
| 13. 02/04/23 | 16:00 | Giresunspor vs Alanyaspor | 2.33 | 3.20 | 2.50 |
| 14. 02/04/23 | 17:30 | Maritimo Madeira vs Boavista Porto | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 15. 02/04/23 | 18:30 | Newcastle United vs Manchester United | 2.39 | 3.20 | 2.80 |
| 16. 02/04/23 | 18:30 | Werder Bremen vs TSG Hoffenheim | 2.23 | 3.45 | 2.85 |
| 17. 02/04/23 | 19:30 | Villarreal CF vs Real Sociedad San Sebastian | 2.28 | 3.05 | 3.10 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 31/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:45 | 1009 | Western Sydney vs Adelaide United | 2.01 | 3.56 | 3.25 |
| 13:00 | 3697 | Kashiwa Reysol vs Urawa Red Diamonds | 3.23 | 3.13 | 2.08 |
| 14:30 | 5145 | Turan Tovuz vs FK Sumgayit | 1.86 | 3.06 | 4.25 |
| 16:00 | 5341 | Neftchi Fargona vs Otmk Olmaliq | 2.55 | 3.05 | 2.36 |
| 16:30 | 4360 | Persepam MU vs PSM Makassar | 2.56 | 3.24 | 2.44 |
| 16:30 | 5157 | PS Tni vs Barito Putera | 2.57 | 3.29 | 2.40 |
| 17:00 | 5418 | Terengganu vs Kelantan United FC | 1.23 | 5.14 | 9.47 |
| 17:45 | 2836 | MC Magra vs US Biskra | 1.94 | 2.95 | 4.09 |
| 18:00 | 1640 | Kolubara vs FK Napredak | 2.62 | 2.98 | 2.54 |
| 18:00 | 1898 | Pribram vs Varnsdorf | 1.88 | 3.39 | 3.54 |
| 18:00 | 3304 | Ararat Yerevan vs Lernayin Artsakh | 1.82 | 3.16 | 4.25 |
| 18:45 | 3084 | Sepahan Esfahan vs Sanat Naft Abadan | 1.20 | 4.50 | 12.00 |
| 19:30 | 3259 | Fortuna Dusseldorf vs Hamburger SV | 2.40 | 3.64 | 2.58 |
| 19:30 | 4017 | Nurnberg vs SV Darmstadt | 3.23 | 3.34 | 2.12 |
| 20:00 | 1942 | Odense vs Midtjylland | 2.88 | 3.49 | 2.27 |
| 20:00 | 3072 | Mladost Lucani vs Novi Pazar | 2.43 | 2.97 | 2.76 |
| 20:30 | 3378 | Bourg Peronnas vs Avranches | 2.14 | 3.16 | 3.32 |
| 21:00 | 1336 | PEC Zwolle vs Jong Utrecht | 1.15 | 6.85 | 12.45 |
| 21:00 | 1544 | VVV Venlo vs NAC Breda | 1.89 | 3.44 | 3.65 |
| 21:00 | 1988 | AL Bataeh (UAE) vs Ajman Club | 3.09 | 3.50 | 2.00 |
| 21:00 | 2667 | Maastricht vs FC Eindhoven | 2.76 | 3.44 | 2.26 |
| 21:00 | 2849 | ADO Den Haag vs Telstar | 2.05 | 3.38 | 3.22 |
| 21:00 | 4079 | FC Oss vs Helmond Sport | 2.45 | 3.23 | 2.66 |
| 21:00 | 4494 | AL Wahda Scc (UAE) vs Al Sharjah SC | 2.47 | 3.28 | 2.50 |
| 21:00 | 5039 | Heracles Almelo vs Almere City | 1.71 | 3.70 | 4.17 |
| 21:15 | 4395 | FC Thun vs AC Bellinzona | 1.46 | 4.21 | 5.34 |
| 21:30 | 1753 | Nieciecza KS vs Ruch Chorzow | 2.15 | 3.18 | 3.02 |
| 21:30 | 3103 | Eintracht Frankfurt vs VfL Bochum | 1.51 | 4.10 | 5.41 |
| 21:30 | 3218 | Genoa vs Reggina | 1.65 | 3.46 | 5.14 |
| 21:30 | 4501 | GKS Piast Gliwice vs Gornik Zabrze | 1.93 | 3.08 | 3.75 |
| 21:30 | 5109 | SV Lafnitz vs SKN St Polten | 3.01 | 3.32 | 2.14 |
| 21:45 | 1207 | Cork City vs Drogheda Utd | 2.08 | 3.23 | 3.13 |
| 21:45 | 2070 | Dundalk FC vs Shamrock Rovers | 3.35 | 3.19 | 2.01 |
| 21:45 | 2657 | St Patricks vs UCD Dublin | 1.22 | 5.15 | 10.09 |
| 21:45 | 3883 | Bala Town vs Gap Connahs Quay | 2.59 | 3.22 | 2.48 |
| 21:45 | 4071 | Shelbourne vs Derry City | 3.94 | 3.12 | 1.86 |
| 21:45 | 4719 | Cardiff Met Uni. vs Penybont | 2.85 | 3.31 | 2.24 |
| 21:45 | 4937 | Arbroath vs Ayr United | 2.92 | 3.23 | 2.26 |
| 21:45 | 5290 | Tranmere vs Harrogate | 2.13 | 3.18 | 3.18 |
| 21:45 | 5912 | Zulte Waregem vs Royal Antwerp | 4.02 | 3.82 | 1.74 |
| 22:00 | 1560 | River Plate (URU) vs Danubio FC | 2.37 | 3.13 | 2.72 |
| 22:00 | 2421 | Levante vs Zaragoza | 1.72 | 3.30 | 4.89 |
| 22:00 | 2482 | Estudiantes FC vs CD Hermanos Colmenarez | 2.09 | 3.09 | 3.24 |
| 22:00 | 3592 | Marseille vs Montpellier | 1.42 | 4.39 | 6.39 |
| 22:00 | 4859 | Burnley vs Sunderland | 1.44 | 4.29 | 6.19 |
| 22:00 | 5773 | Mallorca vs Osasuna | 2.19 | 2.80 | 3.60 |
| 22:15 | 3486 | Ghazl EL Mahallah vs El Ittihad Alexandria | 3.37 | 3.02 | 2.19 |
| 22:15 | 4349 | GD Estoril vs Gil Vicente | 2.66 | 3.21 | 2.51 |
| 22:15 | 5799 | Farco FC vs Aswan | 2.30 | 2.80 | 3.40 |
| 23:00 | 5298 | Deportivo Municipal vs Sporting Cristal | 5.05 | 3.40 | 1.62 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# WAPINZANI SIMBA, YANGA CAF HADHARANI JUMATANO

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba na Yanga watawafahamu wapinzani wao wa mechi za hatua ya robo fainali ifikapo Jumatano, imefahamika.

**Droo hiyo itakayochezeshwa na maofisa wa CAF itafanyika Cairo, Misri kuanzia saa 12:30 usiku kwa saa za Tanzania.**

Simba ambayo imetinga hatua ya robo fainali baada ya kushika nafasi ya pili katika Kundi C leo usiku itacheza mchezo wa kukamilisha ratiba dhidi ya wenyeji, Raja Casablanca na kuna uwezekano mkubwa kukutana na timu za JS Kabylie ya Algeria au Wydad Casablanca ya Morocco ambazo kila moja ina pointi 10 na iko katika Kundi A.

Pia Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini au Al Hilal ya Sudan, atakayeongoza Kundi B mara baada ya mechi za mwisho, ama Esparance ya Tunisia au CR Belouizdad ya Algeria anaweza kukutana na Simba.

Kwa upande wa Yanga ambayo inakwenda kucheza mechi yake ya mwisho ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe jijini Lubumbashi, ndiyo itakayoamua kama itamaliza ya kwanza au wa pili.

Yanga ambayo inaongoza kundi hilo kwa idadi ya mabao ya kufunga ina pointi 10 sawa na US Monastir ya Tunisia inayoshika nafasi ya pili.

Hata hivyo, wawakilishi hao wa Tanzania ambao wapo Kundi D, huenda wakakutana na Malumo Gallats ya Afrika Kusini au USM Alger ya Algeria kutoka Kundi A, River United ya Nigeria au ASEC Mimosas ya Ivory Coast kutoka Kundi B, ASFAR Rabat ya Morocco au Pyramids na Future zote za Misri.



Wachezaji vijana wa mpira wa magongo wakifanya mazoezi ili kujiweka sawa katika viwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park, Dar es Salaam jana. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Yanga ya wasomi yaitisha Mazembe

INATOKA UKURASA 24

timu yao ikitoa burudani na shangwe la kimataifa linahamia ugenini," alisema Kaze.

Wakati huo huo, Kiungo wa Yanga, Mudathiri Yahya, ambaye juzi aliongeza mkataba wa miaka miwili kuitumikia timu hiyo kwa misimu ijayo, alisema ataendelea kupambania ili wafikie malengo.

"Nitachowaahidi wanachama na mashabiki wa Timu ya Wananchi nitaendelea kujituma ili kuhakikisha ninaipa mafanikio timu yetu. Kwangu ni furaha sana kuwa moja ya wachezaji wa kikosi cha Yanga.

"Tuna mashindano mengi mbele yetu, tuna Ligi Kuu ambayo tunahitaji kutetea ubingwa, tuna michuano ya CAF na FA yote wachezaji tumedhamiria kupambana na kuipa mafanikio klabu," alisema Mudathir.

Yanga ndio kinara wa Kundi D ikiwa na pointi 10 sawa na US Monastir ya Tunisia, Real Bamako ya Mali inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi tano wakati TP Mazembe inaburuta mkia ikiwa na pointi tatu.

# Simba: Tunahitaji heshima

INATOKA UKURASA 24

hivyo tumekuja huku kwa lengo moja kulinda heshima ya klabu na taifa kwa ujumla, hatutaki kuingia kwenye rekodi mbaya ya kupoteza, au kupoteza kwa idadi kubwa ya mabao," alisema meneja huyo.

Aliongeza hawataidharau mechi hiyo kwa sababu bado wanaitumia kama njia ya kujenga timu kuelekea hatua inayofuata ya mashindano hayo.

Simba itashuka uwanjani katika mechi hiyo ikiwa kwenye nafasi ya pili na pointi tisa mkononi huku wenyeji wakiwa ni vinara wa kundi hilo baada ya kujikusanyia pointi 13 kibindoni.

Matokeo yoyote katika mechi hiyo hayatabadilisha msimamo wa kundi wakati Horoya ya Guinea na Vipers ya Uganda nao watakutana katika mechi nyingine ya mwisho ya kukamilisha ratiba.

Baada ya mechi hiyo kumalizia, Simba itarejea nchini kusubiri kufahamu mpinzani wake wa hatua ya robo fainali katika droo itakayochezeshwa Jumatano huko jijini Cairo, Misri.

# Michezo

Ijumaa Machi 31, 2023

Nipashe




'Sijashinikiza kulipwa mshahara mnono'

UKURASA 21





Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, akizungumza kuhusu mikakati mbalimbali ya serikali katika mkutano maalumu wa wadau wa sekta hiyo uliofanyika kwenye Ukumbi wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga ya wasomi yaitisha Mazembe

**Na Saada Akida**

WAKATI ikiwapa mikataba mipya wachezaji wake ambao inawahitaji kuendelea kupata huduma yao, Yanga imeahidi kutobweteka katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe itakayochezwa keshokutwa mjini Lubumbashi.

Kikosi cha Yanga kiliwasili salama Lubumbashi tayari kwa mechi hiyo ya kuweka heshima kwa kila upande.

Hata hivyo, vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga itawakosa nyota wake kadhaa ambao ni pamoja na Bernard Morrison, Denis Nkane, Abdultwalib Mshery, Dickson Ambundo na Crispin Ngushi kutokana na kuwa majeruhi.

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kusafiri, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wanatambua mchezo huo utakuwa mgumu lakini wao wanahitaji pointi tatu ili kufikia malengo.



Kaze (pichani) alisema anaamini wachezaji watakaopata nafasi ya kucheza wataonyesha kiwango kizuri huku wakisahau matokeo ya mechi ya kwanza walipowakaribisha kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Aliwataja wachezaji ambao watawakosa ni golikipa chaguo la kwanza, Djigui Diarra na kiungo, Khalid Aucho kutokana na kutumikia adhabu za kadi tatu za njano.

"Tuna mchezo dhidi ya TP Mazembe, tunakumbuka tulipocheza nao hapa (Dar es Salaam) tulishinda, sasa tunawafuata tukiwa na ari ile ile ya kusaka ushindi na kupata pointi tatu muhimu.

Mashabiki tunatambua umuhimu wao na kuja kwao kutaongeza nguvu, ndio maana tumewapa fursa ya kwenda kuiona

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba: Tunahitaji heshima

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Ni katika mechi ya 'usiku mkubwa' dhidi ya Raja Casablanca ambayo...

HUKU ikiwa na tiketi ya kucheza robo fainali mkononi, Simba imepanga kucheza kwa kiwango cha juu katika mechi yake ya kukamilisha ratiba ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji, Raja Casablanca itakayochezwa 'usiku mkubwa' wa leo kwenye Uwanja wa Mohammed V nchini Morocco.

**Kundi la pili la wachezaji wa timu hiyo limeshawasili Morocco tayari kwa mechi hiyo ambayo Wekundu wa Msimbazi wataitumia pia kama sehemu ya maandalizi ya hatua inayofuata ya mashindano hayo ya kimataifa.**

Kocha Mkuu wa Simba, Robert Oliviera 'Robertinho' alisema kikosi chake sasa ni imara tofauti na kilivyokuwa wakati wanakutana katika mechi ya kwanza na Raja Casablanca.

Robertinho alisema pia yeye alikuwa na siku chache tangu alipojiunga na kikosi hicho, hivyo muunganiko wa timu ulikuwa bado haujakaa vyema.

"Tumeimarika idara zote, wanakutana na kikosi tofauti na kile cha mechi ya mkondo wa kwanza, wasitarajie mteremko, tunahitaji kushinda ili kumaliza kwa heshima, lakini tukionyesha ubora wetu," Robertinho alisema.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili jana wamejiandaa vizuri na wamekwenda Morocco kwa ajili ya kulinda heshima ya klabu na taifa la Tanzania.

Rweyemamu alisema mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa kila upande kwa sababu wenyeji wanataka kuendeleza ubora wao na Simba imejiimarisha kupindua meza.

Meneja huyo aliongeza hawatakubali kupoteza tena mechi hiyo ya marudiano na ndio sababu kubwa wamejiandaa kucheza kwa nguvu zote tofauti na baadhi ya wadau wanavyofikiri.

Alisema wamezungumza na wachezaji na kuwakumbusha hawataki kuingia katika rekodi mbaya kama ambayo ilivyotokea misimu iliyopita, hivyo watashuka dimbani kupambana kama vile bado hajawatinga hatua ya robo fainali.

"Kila kitu kimeenda sawa, kikosi cha pili kimewasili kwa ajili ya mechi ya mwisho. Tulipokwama Arusha kuna baadhi ya wachezaji walirejea Dar es Salaam na kesho yake wakaungana na wenzao waliobaki katika kikosi cha Taifa Stars wakaondoka nao, baada ya kufika Doha, Qatar wakakutana na wachezaji wengine ambao walikuwa wametoka kuzitumikia nchi zao, wakapanda ndege moja na kuwasili hapa, kwa hiyo kikosi kimekamilika.

Kimsingi tumekuja katika mechi ya mashindano, kwa bahati mbaya tulipoteza mechi iliyopita kwa mabao 3-0,

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >